# Nipashe

Jumanne Agosti 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581781

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**TAZAMA** yatoa gawio Bil. 4.3/- kwa serikali

UKURASA 2



**Viwanda** vyafungwa kwa ukosefu wa bidhaa

UKURASA 4



**ZRA** yabaini ufisadi leseni uingizaji wa vileo Zanzibar

UKURASA 17

**MABAO KWA MBAPPE YATAKUJA - ANCELOTTI**

UKURASA 21



# Lissu ahofu pesa chafu kupenyezwa CHADEMA

- **Ashangaa** matumizi makubwa, asema alifuatwa nyumbani na kitita...

*Endelea ukurasa 2*

UKURASA 3

## Mpango aagiza udhibiti wa magari ya wanafunzi






Wataalamu Bingwa wa Upasuaji Nyonga na Magoti wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) – Mloganzila, wakimfanyia upasuaji wa magoti mgonjwa. Hospitali hiyo imeanza kufanya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 30 kwa ushirikiano wa Daktari Bingwa Mbobezi kutoka India, Dk. Venuthuria Ram Mohan Reddy, kwenye kambi maalumu ya upasuaji kuanzia jana. **PICHA: MNH-MLOGANZILA**

## Watoto sita, watatu wa familia moja walivyokufa maji wakati wakiogelea

UK. 3

**MICHEZO** **FADLU AKOSHWA NA MUKWALA, MASHAKA** UK.24

**MAONI,** UK.6



Mjasiriamali kutoka kikundi cha mapishi cha Utulivu Cataring kilichoko Mtaa wa Masaki wilayani Muheza mkoani Tanga, Joyce Ernest (kulia), juzi akitoa elimu ya mapishi kwa wajasiriamali wenzake, ambapo kikundi hicho kimeomba kupatiwa mkopo wa fedha kutoka halmashauri. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Lissu ahofu fedha kupenyezwa CHADEMA

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameonesha hofu ya kupenyezwa fedha ndani ya chama hicho ndiyo maana alilazimika kukemea suala la rushwa sababu alihisi kuna fedha zinaingizwa kutoka serikalini.

Kutokana na hofu hiyo, amesema kuna uwezakano jambo hilo likakivunja nguvu chama kutetea haki za Watanzania.

Lissu aliyasema hayo jana katika mahojiano na kipindi cha Dakika 45 kilichorushwa na kituo cha televisheni cha ITV huku akisisitiza kuwa alilazimika kukemea jambo hilo ili kuonesha ukubwa na madhara ya tatizo hilo ndani ya chama.

Alisema alishtuka kuona katika kipindi cha uchaguzi, chama hicho kinakuwa na fedha ambazo hazijawahi kuwapo wala kutumika katika shughuli za kawaida za chama na kuhisi kuwa pengine zinatoka serikalini kama rushwa.

Pia, suala lingine lililompa shaka ni kufuatwa na watu na kumtaka abadilishe msimamo wake juu ya mambo anayoyakosoa anapokuwa kwenye hadhara, jambo ambalo halijawahi kutokea kwake tangu aingie kwenye siasa.

Kwa mujibu wa Lissu, suala hilo lilimpa shaka na kujiuliza maswali mengi na kumpa wasiwasi kuwa kama chama kinaruhusu rushwa, kuna uwezekano wa kukivunja nguvu ya utendaji kazi hasa katika kipindi ambacho nchi ina changamoto nyingi zinazohitaji kutatuliwa.

"Kama wanaweza kunifuata mimi nyumbani wakakaa na kuniambia hivi, nitakuwa niko peke yangu kweli? Nilijiuliza maswali mengi kwa hiyo sikwenda kuropoka kwenye mkutano wa hadhara. Kuna tatizo na linahitaji lisemwe hadharani ili lisikichafue chama chetu," alisema.

Alisema maneno yanayoendelea kuwa kuna migongano ndani ya chama hicho ni ya kawaida hasa katika kipindi hiki ambacho wanafanya uchaguzi wa ndani ule wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu, na uchaguzi mkuu Oktoba 2025.

"Katika uchaguzi wowote wanachama wanatafuta nafasi wawe viongozi wa chama. Wengine wanatafuta nafasi wawe wagombea wa chama na wawakilishi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, udiwani, ubunge na urais. Kwa hiyo, katika mwaka wa uchaguzi wa aina hii kusipokuwa na kelele hizo sio chama cha siasa," alisema.

Kwa miaka 20, alisema amekuwa na uhusiano mzuri na Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe, na hawajawahi kugombana wala kuvunjiana heshima.

Alisema tofauti za misimamo ya kisiasa kati yao zipo na ni jambo la kawaida kwa sababu wao ni watu wenye mitizamo tofauti lakini kuna watu wanataka suala hilo lionekane kuwa ni ugomvi.

"Kwa mfano tunatofautiana kwenye suala la maridhiano. Mimi nadhani kwamba hili suala halitofika popote ni uongo tu, ni namna tu ya kupunguza joto na kukonga nyoyo za jumuiya za kimataifa ili serikali ipate jina zuri na misaada wakati mwenyekiti (Mbowe) alisema kupitia maridhiano tutafika," alisema.

Kwa mujibu wa Lissu, kama wapinzani wanadhani chama hicho hakitaki maridhiano, wanakosea kwa sababu katika serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati John Magufuli, chama hicho kilitangaza hadharani kutaka maridhiano na serikali ili wazungumzie wimbi la watu kutekwa lililokuwa linaendelea. "Tulipaza sauti ya maridhiano na Rais (Magufuli) alipogundua kwamba kufungulia watu kesi za uongo za ugaidi hakumlipi, akasema sasa tuzungumze. Tulipeleka mapendekezo yetu, juu ya mambo yanayohitajika kufanywa ili nchi iwe na maridhiano ya kweli, wameyakataa yote," alisema.

Kuhusu kauli aliyoitoa hivi karibuni kuwa chama hicho si baba yake, alisema alikuwa na maana kuwa alihamia katika chama hicho kwa sababu alivutiwa na sera na itikadi na ikitokea mambo hayo yakabadilika, anaweza kuondoka.

"CHADEMA ni chama cha siasa na tunaunganishwa na itikadi fulani chenye mipango, sera, misimamo fulani, ikiondoka hiyo tutakutana kwenye urafiki wa mambo mengine lakini si masuala ya siasa," alisema.

**KUANZISHA CHAMA**

Kuhusu uvumi kwamba ana mpango wa kuanzisha chama, alisema hana mpango huo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mtazamo wake juu ya sera ya vyama vya siasa na ofisi ya msajili wa vyama kuwa vimewekwa kudhibiti upinzani.

"Mimi nianzishe chama halafu Jaji (Francis) Mutungi (Msajili wa Vyama vya Siasa) akisajili? Eeh itabidi tusubiri karne nyingine. Sijafikiria kuanzisha chama kingine wala kuhama CHADEMA na sababu ndizo hizo," alisema.

Alisema licha viongozi wa chama hicho akiwamo yeye kuongoza kushtakiwa kwa uchochezi hajawahi kukutwa na hatia hata mara moja na hakuna kesi iliyofika mwisho.

**SERA MPYA YAJA**

Kwa sasa, Lissu alisema chama hicho kiko kwenye mchakato wa kutengeneza sera ya jinsia na makundi maalum ikiwa ni maelekezo kutoka katika Sheria ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa maboresho hivi karibuni.

Alisema kuna haja ya kuangalia upya sheria ya vyama vya siasa kipengele cha vigezo vya chama kupata ruzuku ili chama kipewe ruzuku kulingana na asilimia ya wabunge wa majimbo, madiwani iliyopata.

"Kama fungu lote ndio asilimia 100 ya kura kwa nini chama kinachopata asilimia moja kisipate ruzuku, kwa nini inaanzia asilimia tano tu? Mimi nahisi kuna ufisadi unaendelea hapo," alisema.

Alisema kwa sheria ilivyo sasa chama kitapata ruzuku kama katika uchaguzi uliopita kilipata wabunge wa majimbo, madiwani wa kata au asilimia tano au zaidi ya kura zote halali zilizopigwa kwa wabunge jambo analodhani kuwa si sawa kwa vyama vingine vya siasa.

**KUIBURUZA TUME KORTINI**

Alisema chama hicho kimepanga kwenda mahakamani ili kujua msimamo wa Tume ya Uchaguzi juu ya ushiriki wa Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi iliyotungwa hivi karibuni imewanyang'anya mamlaka hiyo.

Alisema katika marekebisho ya sheria za uchaguzi mwaka huu kulitungwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi yenye kipengele kinachoeleza kuwa tume hiyo ndio yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa vijiji na wa mitaa kwa kufuata utaratibu utakaowekwa kwenye sheria itakayotungwa na bunge.

Alisema kwa maana hiyo TAMISEMI na waziri wake, Mohamed Mchengerwa, hawana mamlaka ya kusimamia uchaguzi huo, hivyo wanashangazwa kuona kuwa waziri huo anatoa tangazo la uchaguzi.

Alisema pia ametia nia kugombea nafasi ya rais wa Tanzania kwenye chama chake hivyo kama vikao vya chama vikimpitisha atawania kiti hicho.

# TAZAMA yatoa gawio bil. 4.3/- kwa serikali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepokea gawio la Sh. bilioni 4.35 kutoka Shirika linalosimamia bomba la mafuta kutoka Tanzania kwenda Zambia (TAZAMA).

Akizungumza wakati wa kupokea hundi ya gawio hilo jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko, alisifu hatua hiyo kuwa ni muhimu kwa Tanzania kwa kuwa mradi wa bomba hilo una miaka mingi na sasa matunda yanaonekana.

"Mara ya mwisho kutoa gawio kwa serikali ilikuwa miaka mitano iliyopita na sasa tumepokea fedha hizi, tunajivunia maana badala ya kuja na sababu na visingizio kadha wa kadha, lakini mmekuja na fedha, kuna baadhi ya taasisi wanakuja na maneno mengi ya kijanja...unajua kulikuwa na Covid, tatizo la dola, lakini nyie hamkuwa hivyo, tunatarajia wakati mwingine kutakuwa na habari njema zaidi," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan alipotembelea Zambia, moja ya maelekezo yake ilikuwa ni miradi inayounganisha nchi hiyo na Tanzania isimamiwe vizuri ili ilete manufaa kwa nchi zote.

Alisema Samia alielekeza kwamba angefurahi kuona miradi kama TAZAMA inaleta siyo tu manufaa ya kikodi kwa nchi bali ichangie kunufaisha maisha ya watu.

Aliipongeza bodi na uongozi wa TAZAMA kwanza kwa kufanya jambo hilo liwezekane.

Aidha, Wizara ya Nishati iko kwenye mazungumzo ili kuongeza uwekezaji kwenye bomba la TAZAMA.

"Kama mnavyofahamu tunataka kupanua bomba lililopo kutoka nchi nane hadi 12 na litaanza muda si mrefu ili tusafirishe mafuta mengi kwenda Zambia na baadaye kutoka Zambia kwenda nchi za Kongo (DRC) na majirani zetu," alisema.

Alisema wanakusudia kuanza ujenzi wa bomba jipya la inchi 24 na kwa sasa wapo kwenye hatua mbalimbali za ununuzi ili mafuta mengi zaidi yasafirishwe kwa bomba badala ya malori.

"Tunataka tuwe na vituo njiani kutokea hapa kwetu katikati kuwe na vituo vingi vya kutoa hayo mafuta mbadala yanayokwenda Kusini yapelekwe na lori sasa litumike bomba lengo letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata mafuta bei nafuu sababu sehemu ya gharama kubwa inayosababisha bei kuongezeka pamoja na nyingine, lakini gharama za usafirishaji zinavyoendelea kuwa kubwa na kufanya mafuta yaendelee kuwa na bei kubwa," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, alisema kuwa gawio hilo linadhihirisha namna ushirikiano wa Tanzania na Zambia ulivyo imara.

Awali, Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu aliisifu TAZAMA na kusema sasa imeamka ikiwa na miaka takriban 58 tangu kuanzishwa.

Mchechu, alisema umri huo kama ni mtumishi wa umma amebakiza miaka miwili kustaafu na kwamba anakuwa kidogo mnyonge mnyonge.

"Lakini kwa TAZAMA badala ya kuwa mnyonge ndio imekuja juu, imekuwa tofauti kidogo," alisisitiza.

Alisema mafanikio hayo ya TAZAMA ni moja ya faida za falsafa ya 4R za Rais Samia akimaanisha maridhiano, ustahamilivu, mageuzi na ujenzi mpya.

Mchechu, alisema mabadiliko ni makubwa kwa sababu yamekuwa kwa mpigo. "Kama mnavyoona na sisi tunatumia mageuzi na ujenzi mpya hapa napenda tumpongeze Rais Samia," alisema Mchechu.

TAZAMA ilitoa gawio hilo kwa serikali jana baada ya kupita miaka mitano. Kwa mara ya mwisho ilitoa Sh. milioni 681.8 mwaka 2019.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, akimsikiliza Mhariri wa Habari wa ITV, Stephen Chuwa, alipotembelea kituo hicho Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Wa tatu kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mpango ataka udhibiti 'school bus'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo saba kwa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, mojawapo ni kuongeza udhibiti kwa magari yanayobeba wanafunzi (School bus), kwamba mengi hayakidhi vigezo vya kutembea barabarani na madereva wake wengi hawana weledi.

Agizo lingine ni wafuatilie ukaguzi wa mara kwa mara kwa magari yote, kufanya ukaguzi mara nne kwa mwaka.

Alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani na miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma.

"Jeshi la Polisi linapaswa kuongeza udhibiti wa mabasi ambayo yamekuwa yakitumika kubeba watoto wa shule, kwani mengi hayana sifa ni mabovu na mengine yanabeba watoto zaidi ya uwezo wake, lakini pia madereva wake wengi hawana weledi," alisema Dk. Mpango na kuongeza:

"Madereva hao wamekuwa wakisababisha ajali za ovyo kama ile iliyotokea Aprili 12, mwaka huu, kule Arusha ambapo wazazi walipoteza watoto wao saba kwa uzembe. Ninawataka Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa dereva anayepewa leseni lazima awe amekidhi vigezo vyote".

Dk. Mpango alisema Jeshi la Polisi linapaswa kutoa elimu ya usalama barabarani mara kwa mara ikiwamo kutanuliwa kwa makundi yote.

Kadhalika, aliwataka wananchi kuwa sehemu ya kukemea uvunjifu wa matukio ya ajali barabarani na siyo kukaa kimya.

"Jeshi la Polisi tumieni Tehama katika kukabili matukio ya usalama barabarani pia mwongeze udhibiti kwenye mabasi ya shule ambayo yamekuwa yakitumika kubeba wanafunzi, lakini mengi hayana sifa ya kutembea barabarani," alisema Dk. Mpango.

Agizo lingine alilitaka Jeshi la Polisi kuwapa ajira zaidi madereva wanawake kwa sababu takwimu zinaonyesha matukio mengi ya ajali yanasababishwa na madereva wanaume kuliko wanawake.

Kadhalika aliwata watumiaji wa barabara wote wazingatie usafi wa mazingira, kwamba lisiwe jukumu la kikundi cha watu.

Aidha, alisema madereva wote wanaovunja sheria wanapaswa kuchukuliwa hatua kali bila kujali kuwa ni dereva wa serikali au binafsi.

Pia, alilitaka Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kuendesha doria za kushtukiza za kufanya ukaguzi wa magari pamoja na weledi wa madereva na wasiokidhi vigezo kuwachukulia hatua kali za kisheria.

> **"Jeshi la Polisi linapaswa kuongeza udhibiti wa mabasi ambayo yamekuwa yakitumika kubeba watoto wa shule, kwani mengi hayana sifa ni mabovu na mengine yanabeba watoto zaidi ya uwezo wake, lakini pia..**

Dk. Mpango alisema kwa hali ilivyo sasa kama hatua madhubuti za kudhibiti ajali hazitachukuliwa utafiti unaonyesha kuwa ajali ndiyo itakuwa chanzo kikuu cha vifo ifikapo mwaka 2030.

"Taifa letu linapoteza nguvu katika kipindi cha mwaka 2023 katika ajali 1,733 zilizotolea vifo vilikuwa ni 1,647 na majeruhi ni 2,716, hivyo kama hatutachukua hatua basi ajali ndiyo itakuwa chanzo kikuu cha vifo ifikapo 2023," alisema.

Kadhalika alisema ajali za pikipiki hivi sasa nchini zinaongezeka ambapo kwa kipindi cha mwaka 2023 zilikuwa 435, kusababisha vifo 376 ukilinganisha na vifo 332 kwa mwaka 2022. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema katika kukabiliana na matukio ya ajali nchini wizara imetekeleza miradi mbalimbali ambayo itasaidia kupunguza hali hiyo.

Alisema moja kati ya miradi hiyo ni pamoja na ule wa miji salama wa kufunga kamera za usalama kwenye miji ambao utekelezaji wake upo katika hatua za mwisho.

Alisema mradi huo utakwenda kutekelezwa kwenye majiji ya Dodoma, Arusha, Mwanza na Dar es Saalam.

"Ni matumaini yetu kuwa miradi hii ikikamilika tutakwenda kudhibiti ajali hasa katika maeneo yasiyo na askari kutokana na kamera zitakazokuwa zimefungwa katika maeneo hayo," alisema Masauni.

Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema moja ya sababu ya kuongezeka kwa ajali barabarani ni makosa ya kibinadamu.

"Baadhi ya madereva hawazingatii masuala ya sheria za usalama barabarani, hivyo kufanya makosa ya kibinadamu na kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la ajali nchini kutokana na hali hiyo baraza tumeandaa mkakati utakaoshirikisha wadau wote na baada ya miezi tutafanya tathmini kuona hali ikoje," alisema Sillo.

Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Cumillius Wambura, alisema katika kukabiliana na ajali nchini wametekeleza maagizo mbalimbali ya serikali ikiwamo kufunga mifumo ya kisasa kudhibiti ajali barabarani.

# Watoto sita, watatu familia moja walivyokufa maji wakiogelea

**Na Ambrose Wantaigwa,** RORYA

WANAFUNZI sita wa Shule ya Msingi Ochuna wilayani Rorya, mkoani Mara wamekufa maji baada ya kuogelea katika bwawa la skimu ya kilimo cha umwagiliaji.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka, alisema watoto hao walifikwa na umauti wakiogelea katika bwawa hilo na watatu kati yao ni wa familia moja.

"Walikuwa watoto saba, mmoja aliondoka bwawani hapo kabla ya tukio, huku wengine wakiendelea kuogelea na kisha kunasa kwenye tope na kupoteza maisha. Wananchi kwa kushirikiana na wazamiaji waliokuwa karibu na eneo hilo walifanikiwa kuopoa miili hiyo," alisema Chikoka.

Kutokana na tukio hilo, Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa rambirambi ya Sh. milioni 30 kwa familia za watoto hao ili kufanikisha mazishi.

Akikabidhi rambirambi hiyo, Chikoka alisema Rais Samia ameguswa na msiba huo na kuwa yuko pamoja na familia za wafiwa hao katika kipindi hicho kigumu.

Chikoka alisema serikali imeagiza wasimamizi wa bwawa hilo kuchukua hatua za haraka kuzuia matukio ya kusababisha kupotea maisha bila sababu, ikiwa ni pamoja na kuweka uzio kuzunguka eneo hilo.

Alisema lazima wazazi na walezi wahakikishe wanalinda usalama wa watoto wao kwa kuwazuia kwenda maeneo hatarishi kama vile katika mabwawa na kina kirefu cha Ziwa Victoria linalopakana na wilaya hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ochuna walipokuwa wanasoma watoto hao, Richard Mahe, alisema wanafunzi wawili kati yao walikuwa wanasoma darasa la sita na walikuwa na uwezo mkubwa kitaaluma.

Alisema shule hiyo na jamii kwa ujumla imepoteza nguvu kazi kwa kuwa wanafunzi hao walikuwa na ndoto za kulitumikia taifa kwa njia mbalimbali baada ya kuhitimu masomo yao.

Aidha, alitangaza mapumziko ya siku moja shuleni hapo ili kuwezesha wanafunzi na walimu kuungana na familia hizo katika kutoa heshima zao za mwisho kwenye mazishi ya pamoja.

# Watendaji uchaguzi wapewa somo uboreshaji daftari la wapigakura

**Na Waandishi Wetu**

WATENDAJI wa uchaguzi katika mikoa ya Mara, Simiyu na Manyara wametakiwa kutoa ushirikiano kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) na wadau wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kufanikisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Mwenyekiti wa INEC, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jacobs Mwambegele, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa watendaji wa uboreshaji ngazi ya mkoa na halmashauri yaliyofanyika Musoma mkoani Mara.

Jaji Mwambegele alisisitiza kuwa ni muhimu kwa watendaji hao kuhakikisha wanafuata maelekezo ya Tume na kushirikiana kikamilifu ili kuhakikisha uboreshaji unafanyika kwa ufanisi.

"Ninawasihi muwe na ushirikiano mzuri na wa karibu na tume wakati wote mtakapokuwa mnatekeleza majukumu yenu. Ikiwa mnahitaji ufafanuzi au maelekezo yoyote, msisite kuwasiliana na tume," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa INEC, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mbarouk Salim Mbarouk, ambaye alifungua mafunzo kama hayo mkoani Simiyu, aliwataka watendaji hao kutoa ushirikiano kwa mawakala wa vyama vya siasa, asasi za kutoa elimu ya mpigakura na waangalizi.

Mkoani Manyara, mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi ngazi ya mkoa yalifunguliwa na Mjumbe wa INEC, Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari, ambaye amewataka watendaji hao kuzingatia mafunzo hayo ili kuwafundisha maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata.

"Mafunzo haya yanawajengea umahiri wa kuwafundisha maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata ili nao wakatoe mafunzo hayo kwa waendeshaji wa vifaa vya bayometriki na waandishi wasaidizi ambao ndio watakaohusika na uandikishaji wa wapigakura vituoni," alisisitiza.

Kufanyika kwa mafunzo hayo ni maandalizi ya kuanza kwa mzunguko wa nne wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ambao unajumuisha mkoa wa Mara, Simiyu na baadhi ya halmashauri za mkoa wa Manyara ambazo ni Mji Babati na Wilaya za Babati, Hanang na Mbulu.

Uboreshaji huo utaanza Septemba 4 hadi 10, mwaka huu na vituo vitakuwa vinafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

# Viwanda vyafungwa kwa uhaba wa samaki

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAZAO ya samaki katika Ziwa Victoria yameshuka kwa asilimia 30 kati ya mwaka 2018 hadi 2020 hatua ambayo imesababisha kufungwa kwa baadhi ya viwanda.

Katibu Tawala Msaidizi Sekta ya Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mwanza, Emily Kasagara, alisema hayo jana katika mkutano wa kuhamasisha wadau wa uvuvi kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Victoria. Kasagara alisema ongezeko la uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali Kanda ya Ziwa imesababisha kushuka kwa mazao hayo na viwanda vingi vya uchakataji wa minofu ya samaki vimepungua.

"Viwanda hivyo vimepungua kutoka 15 hadi vinane. Hatua hiyo imetufanya kuchukua hatua mbalimbali zikiwamo kusimamia sheria za uvuvi endelevu, udhibiti wa zana za uvuvi haramu na kuwashirikisha wadau wote wa uvuvi kulinda mazalia ya samaki," alisema.

> **"Viwanda hivyo vimepungua kutoka 15 hadi vinane. Hatua hiyo imetufanya kuchukua hatua mbalimbali zikiwamo kusimamia sheria za uvuvi endelevu, udhibiti wa zana za uvuvi haramu na kuwashirikisha wadau wote wa uvuvi kulinda mazalia ya samaki," alisema.**

Mkurugenzi wa Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Mohammed Sheikh, alisema licha ya Ziwa Victoria kuchangia asilimia 67 ya uvuvi nchini kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023/24, uvunaji wa samaki unashuka kila uchao kutokana na uvuvi haramu.

Alisema takwimu hizo zinaonesha kuwa, uvunaji wa sangara umeshuka kwa zaidi ya tani 10,000 kutoka tani 91,709 kwa mwaka 2019 hadi tani 80,265 kwa mwaka 2023.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, alisema serikali itaendelea kudhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na wadau wa uvuvi lengo likiwa ni kuhakikisha kuna ongezeko la mazao hayo.

Pia aliwataka wadau kuandaa mikakati mahususi ambayo itasaidia kudhibiti uharibifu wa mazalia ya samaki na kuongeza upatikanaji wa rasilimali hizo kwa uhakika pamoja na serikali za mitaa kuongeza udhibiti katika maeneo yao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa tatu unaanza kufanyika tarehe 21 hadi 27, Agosti, 2024 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 21 na kuhitimishwa Jumanne tarehe 27 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 16 Agosti, 2024 na:**

**Kalima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**


# Wasomi, wataalamu waridhishwa mradi bomba la mafuta EACOP

**Na Kulwa Mzee**

WASOMI na wataalamu mbalimbali nchini wameeleza kuvutiwa na utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP), wakisema umekidhi vigezo vyote vinavyotakiwa kimataifa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wasomi hao wamesema utekelezaji mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga utachagiza maendeleo ya haraka kwa jamii zilizopitiwa na mradi.

Aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu na hatimaye Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Profesa Faustin Kamuzora, alipongeza usimamizi wa mradi huo kuwa na matokeo chanya katika maeneo yote uliopita.

"Huu mradi ni mkubwa na umezingatia taratibu zote za kimazingira na ubora wake ni hali ya juu. Mimi ni mwenyeji wa Kagera na nimefanya kazi kama Katibu Tawala wa mkoa huo ambako mradi umeanzia ukitokea Uganda," alisema Prof. Kamuzora ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine.

Profesa Kamuzora alisema miongoni mwa miradi ambayo ameshawahi kuiona na utekelezaji wake ukiwa wa viwango vya hali ya juu ni wa EACOP ambao umekuwa ni manufaa pia kwa wananchi.

"Mradi wa EACOP nimeufuatilia tangu upembuzi yakinifu unaanza yaani 'feasibility study' yake mpaka hatua hii ya utekelezaji wake," alisema.

Wakili Msomi na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Kampasi ya Mbeya, Dk. Tasco Luambano, alisema mradi wa EACOP ni miongoni mwa mradi inayoiweka Tanzania katika ramani ya dunia.

"Nazipongeza sana serikali za Uganda na Tanzania kukubaliana mradi upite kwenye ardhi ya nchi hizi mbili. Ni mradi ambao ukamilikaji wake utabadilisha maisha kwenye maeneo mradi umepita katika mkoa ile minane," alisema Dk. Luambano.

Mtaalamu wa Oil na Gesi, Jackson Jalimba alizipongeza serikali za Tanzania na Uganda kwa kukubaliana utekelezaji wa mradi huo, kwani una manufaa yake ya kiuchumi na kijamii ni makubwa sana.

Bomba hili linapita katika mikoa nane ya Tanzania Bara ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, likijumuisha wilaya 24, kata 134 na vijiji zaidi ya 180.

Wanahisa wa mradi huu ni TotalEnergies (asilimia 62), kampuni ya mafuta ya Uganda (UNOC) asilimia 15, CNOOC ya China asilimia nane pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) asilimia 15.

WATU KUPOTEA

# Miili mingine yabainika imefukiwa

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU tatu baada ya Jeshi la Polisi kutoa taarifa kuhusu miili ya watu waliotoweka katika mazingira yenye utata, miili mingine ya watu wawili imepatikana, mmoja ukiwa umenyofolewa baadhi ya viungo.

Aprili 24, mwaka huu, jeshi hilo lilitoa taarifa kuhusu matukio ya watu kuripotiwa katika vituo vya polisi kwamba wamepotea katika mazingira yenye utata na baadaye kupatikana wakiwa wameuawa katika mikoa ya Dar es Salaam, Singida na Tanga.

Katika taarifa yake ya jana, jeshi hilo kupitia kwa Msemaji wake, Naibu Kamishna wa Polisi, David Misime, lilieleza kuwa wakati linafuatilia tukio la mkoani Singida, lilibaini miili mingine ya watu wawili ikiwa imefukiwa shimoni.

Alisema kuwa baada ya kukamatwa watuhumiwa Seleman Nyandalu, Said Msanghaa na Nkamba Kasubi ambaye ni mganga wa kienyeji, waliwaongoza polisi na wananchi hadi walikokuwa wamefukia mwili wa Samwaja Said baada ya kumuua.

Kamanda Misime alisema kuwa Agosti 24, mwaka huu, walibaini mashimo mengine mawili ambayo baada ya kufukuliwa, ulipatikana mwili wa Gidion Mnyaro ambaye mara ya mwisho alionekana akiwa amepakizwa kwenye pikipiki na watu wawili Oktoba 15, 2023 na taarifa za kutoweka kwake kuripotiwa polisi.

**Alisema kuwa, mwili mwingine ambao haukutambuliwa, ukihitaji mwendelezo wa uchunguzi wa wataalamu wa kuchunguza maiti na vinasaba (DNA) - una mabaki ya nyonga, paja la mguu wa kulia na kushoto.**

Alisema kuwa, mwili mwingine ambao haukutambuliwa, ukihitaji mwendelezo wa uchunguzi wa wataalamu wa kuchunguza maiti na vinasaba (DNA) - una mabaki ya nyonga, paja la mguu wa kulia na kushoto.

Hata hivyo, Kamanda Misime alisema kuwa mabaki ya miili ya watu hao wawili yalibainika baada ya askari na wananchi kuoneshwa na Asha Bakari (51), mkazi wa Migugu ambaye ni mke wa Awadh Ramadhani (54) ambao ni wakwe wa Kasubi - mganga wa kienyeji anayeshikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za mauaji.

Kamanda Misime anasema ilielezwa kuwa wawili hao waliuawa na mkwe wake huyo akishirikiana na Nyandalu na Awadh, ambaye anatafutwa.

"Imedaiwa chanzo cha Gidioni kuuawa ni kitendo chake cha kuuza shamba mara mbili ambapo aliwauzia Hawa Sumwa (54) na Idd Hussein (25), wakazi wa Makuro lakini baadaye ikabainika shamba hilo alishaliuza tena kwa mtu mwingine," alidai.

Kamanda Misime alisema Hawa na Hussein walifikisha suala hilo kwa mganga huyo wa kienyeji; naye akawaambia ili fedha zao zilirudi, inabidi Gidion atolewe kafara na ndipo mauaji hayo yakapangwa na kufanyika.

"Hadi sasa, kutokana na mlolongo huo wa mauaji, wanaoshikiliwa ni watu saba ambao ni Nyandalu, Msanghaa, Kasubi, Asha, Awadh, Hawa na Idd," Naibu Kamishna Misime alisema.




Kaimu Mkurugenzi wa Wateja wa Awali na Kati wa Benki ya CRDB, Muhumuliza Buberwa (wa pili kulia), akiwa na Meneja Mkazi wa Shirika la Ndege la Qatar, Isaack Wambua, kwenye uzinduzi wa punguzo la bei kwa abiria watakaolipa nauli zao kwa kutumia kadi za Tembocard Visa kuanzia leo (jana) mpaka Oktoba. Uzinduzi huo ulifanyika jana makao makuu ya Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabainika kulima bangi pembezoni mwa hifadhi, sita watiwa mbaroni

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, imewakamata watu sita katika Kijiji cha Nyarutanga, mkoani Morogoro kwa tuhuma za kukutwa na kilo 342 za bangi.

Imesema watuhumiwa hao wamekamatwa baada ya kufanyika operesheni maalum kwa siku tisa katika vijiji vya Nyarutanga, Lujenge na Mafumbo, mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uteketezaji wa mashamba hayo, Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani, taratibu zitakapokamilika.

Alisema kuwa, katika operesheni hiyo wameteketeza ekari 1,165 za mashamba ya bangi pamoja na kukamata kilo 102 za mbegu za bangi.

Lyimo alisema mashamba hayo yalikuwa yamelimwa pembezoni mwa Mto Mbakana, Misigiri na Mgeta kwenye eneo la akiba la Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA).

"Uharibifu mkubwa sana wa mazingira umefanyika katika eneo hili, miti imekatwa ili kupata eneo la kulima bangi na hivyo kuharibu uoto wa asili," alisema.

Kiongozi huyo alisema kumefanyika pia uharibifu katika eneo la akiba la MINAPA, ikiwamo ikolojia ya eneo hilo pamoja na uoto wa asili.

Alishukuru wananchi hususani vijana waliojitolea kushiriki katika uteketezaji mashamba ya bangi kwa kushirikiana na maofisa wa serikali, pia kwa kuiwezesha mamlaka kufanya operesheni hizo.

"Tutajitahidi kutekeleza dhamira ya serikali ya kulinda afya za wananchi kwa kuhakikisha kwamba tunamaliza tatizo la dawa za kulevya nchini, yakiwamo mashamba ya bangi, mirungi pamoja na kudhibiti kemikali bashirifu na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kutumika kama mbadala wa dawa za kulevya," alisema.

Aliomba wananchi wa mkoani Morogoro na mikoa mingine kushirikiana na DCEA kupiga vita kilimo cha bangi na aina nyingne za dawa za kulevya.

Baadhi ya wananchi walioshiriki katika operesheni hiyo, akiwamo Saidi Mijinga, mkazi wa Kisaki, alisema eneo lililotumika kulima bangi ni kubwa, endapo lingetumika kulima mazao mengine, wananchi wangenufaika.

Mwananchi mwingine, Joseph Juma aliomba wenzake kuendelea kufichua wauzaji na wafanyabiashara wa bangi, akisema ina madhara makubwa kwa vijana na jamii.

# CRDB kutoa punguzo katika tiketi za ndege kwa abiria

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB kwa kushirikiana na wabia wake wa kimkakati ambao ni kampuni ya Visa International imetangaza kutoa nafuu ya nauli ya asilimia 22 kwa abiria wa ndege wanaolipia tiketi zao kwa kutumia kadi za Tembocar Visa.

Nafuu hiyo inajumuisha punguzo la asilimia 12 litakalotolewa na kampuni ya Visa International pamoja na asilimia 10 ya fedha taslimu itakayorudishwa katika akaunti ya mteja wa Benki ya CRDB baada ya kulipia tiketi yake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana wakati wa kuzindua kampeni hiyo itakayodumu kwa miezi sita, Mkurugenzi wa Wateja wa Awali na Kati wa Benki ya CRDB, Bonaventura Paul, alisema ushirikiano huo unalenga kuunga utamaduni kwa wateja kutumia kadi kufanya malipo na kuachana na matumizi ya fedha taslimu.

"Punguzo hili la asilimia 22 ni sehemu ya motisha kwa wateja kujenga utamaduni wa kutumia kadi kufanya malipo. Nitumie nafasi hii kuwakaribisha wateja wetu wanaotaka kusafiri kwa ndege ili kunufaika na punguzo hili," alisema Paul huku akibainisha kuwa punguzo hilo pia linatosha kwa abiria kununua zawadi kwa ajili ya wapendwa wao pindi wawapo safarini.

Mkurugenzi huyo alisema ushirikiano wa Benki ya CRDB, Visa International na shirika moja la ndege unazijumuisha taasisi mbili kubwa zenye ubora unaotambulika ndani na kimataifa uliozifanya zitunukiwe tuzo za aina tofauti.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000, Paul alisema Benki ya CRDB imetunukiwa takriban tuzo 200 za ndani na kimataifa ikiwamo tuzo za utoaji wa huduma bora za Visa.

"Benki yetu ndio kiongozi katika ubunifu wa huduma na bidhaa zinazokidhi mahitaji na matarajio ya wateja wetu," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii iungane kukemea rushwa ya ngono nchini

**SUALA** la rushwa ya ngono kwa miaka mingi limekuwa sawa na jambo la kawaida katika jamii ya Watanzania. Hali hiyo inatokana na kuwapo kwa madai ya matendo hayo katika sehemu mbalimbali, hivyo kusababisha jamii hadi taifa kutiwa doa.

Rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia, vimeripotiwa mara kwa mara katika taasisi mbalimbali kuanzia elimu ya sekondari hadi vyuo vikuu, taasisi za kazi za umma na binafsi. Katika elimu ya juu kwa mfano, kumekuwapo madai kwamba baadhi ya wahadhiri na maprofesa wamekuwa wakiwalazimisha wanafunzi wa kike kufanya nao ngono ili kuwawezesha kufaulu mitihani na hatimaye kuhitimu shahada zao.

Hata katika ajira, baadhi ya maofisa waandamizi kwenye wizara na taasisi za serikali na za binafsi wamekuwa wakiwalazimisha wasichana na wanawake kujihusisha nao kimapenzi ili wapate ajira au wapandishwe vyeo.

Kwa wale wanaogoma kufanya hivyo, hukosa ajira hata kama wana sifa zinazostahili. Kwa wale walioko katika ajira, wanapokataa kufanya hivyo, huingia katika manyanyaso na ukatili ikiwamo kutopandishwa vyeo, kuhamishiwa sehemu zinazoonekana hazina manufaa ikiwa sehemu ya kuwakomoa.

Kwa ujumla, suala hilo limekuwa sumu katika maeneo mbalimbali na chanzo cha kupata watu wasio na sifa kuingia katika ajira na uongozi. Pia wale wanaohitimu wanapata alama nzuri kwa kukubali kutumika kingono na matokeo yake wanapatikana watu wasio na uwezo na hatimaye kuzorotesha maendeldo ya taasisi na taifa kwa ujumla.

Hivi sasa, suala hilo limeelezwa kukithiri katika vyama vya siasa kwa viongozi kuwataka wanawake wanaoomba nafasi za uongozi kushiriki na vitendo vya ngono. Wenye sifa za uongozi, wanaokataa kufanya vitendo hivyo hukosa nafasi za uongozi bali wanaopata ni wale wanaokubali kuuza utu wao kwa kushiriki rushwa ya ngono.

Katika mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu mbinu za kupambana na rushwa ya ngono kuelekea uchaguzi, yaliyoandaliwa na asasi ya Sauti ya Jamii Kipunguni, baadhi ya wanawake walisema wamekuwa wakichukua uamuzi mgumu wa kufanya vitendo vya ngono na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ili kupata nafasi za uongozi. Baadhi ya wanawake hao walisema wamekuwa wakilazimika kufanya hivyo na viongozi wao ili kupata nafasi hiyo, vinginevyo inakuwa vigumu kwao kupata uongozi wa kuchaguliwa au kuteuliwa. Walisema unapofika wakati wa uchaguzi, ama wa serikali za mitaa au ule wa Rais, Wabunge na Madiwani, bila kufanya hivyo hawawezi kupata nafasi hizo za uongozi.

Wanawake hao walikwenda mbali zaidi kwa kusema unapokaribia wakati wa uchaguzi, wamekuwa wakilazimika kujipendekeza kwa viongozi wa ngazi za wilaya, mikoa na hata taifa kulingana na nafasi ya uongozi wanayoiomba. Katika kufanya hivyo, wanalazimika kujiingiza kwenye vitendo vya ngono na viongozi hao.

Wahenga wanasema 'mtumikie kafiri upate mradi wako'. Kwa muktadha wa jambo hilo la kupata nafasi ya uongozi kupitia uchaguzi, uteuzi au nafasi ya ajira katika taasisi ya serikali au binafsi, suala hili halikubaliki hata kidogo.

Ni wakati sasa kwa jamii nzima ya Tanzania kusimama na kukemea kwa nguvu zote jambo hilo kwa kuwa linaitia doa taifa. Asasi za kiraia, viongozi wa dini, serikali na jumuiya ya wafanyabiashara, hawana budi kupaza sauti katika kukemea kwa wazi vitendo hivyo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na wasichana.

Kwa wale wanaolazimishwa kushiriki vitendo hivyo ili kupata ajira, kufaulu mitihani na kuteuliwa au kuchaguliwa katika nafasi za uongozi, wanapaswa kupaza sauti kwa kufikisha malalamiko hayo katika vyombo husika. Tanzania bila rushwa ya ngono inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Fuatilieni mienendo ya watoto wenu shuleni

Na Sabato Kasika

**KUMEKUWAPO** na kipande cha video kilichowahi kurushwa mitandaoni kikimwonyesha mwanafunzi akihojiwa baada ya kukamatwa usiku wa manane kwa tuhuma za kujihusisha na uhalifu.

Mtoto huyo alikamatwa maeneo ya Mbezi Msigani Dar es Salaam akijitambulisha kuwa umri wake ni miaka 15 na anasoma kidato cha kwanza katika shule moja ya sekondari ya Dar es Salaam.

Katika mahojiano na watu waliomkamata, akielezea kwa kina jinsi anavyopita, katika miji ya watu usiku wa manane na kuiba kandambili zinazoachwa nje.

Inawezekana video hiyo ni uzushi au ni ukweli ila ninachotaka kusema ni kwamba kuna cha kujifunza.

Ingawa video hiyo haikuonyesha mwisho wa mahojiano, lakini inatosha kuwashtua wazazi na walezi kwamba kuna umuhimu wa kufuatilia mienendo ya watoto wao shuleni na nyumbani.

Wakifanya hivyo, wanaweza kujua mengi kuhusu tabia na mienendo ya watoto, kwani inashangaza kuona mtoto kama huyo hayupo nyumbani usiku wa manane. Inawezekana akachukua madaftari akasema anakwenda kusoma 'twisheni' kwa rafiki yake, na kueleza kuwa atakesha huko, lakini ni vyema mzazi kujiridhisha badala ya kukubali tu.

Pamoja na hayo, ni vizuri mzazi au mlezi kuwajua marafiki wa mtoto wake kuwa ni kina nani na wana tabia gani ili kama si wema, basi amwepushe nao.

Si sahihi kumruhusu mtoto kwenda katika mazingira ambayo wewe mzazi huyajui kwa sababu ya kuaga kuwa anakwenda 'twisheni'.

Ninaamini wapo wanaotumia ujanja huo kuwaaminisha wazazi kuwa wanasoma, na kumbe si kweli.

Wanaodanganywa kwa njia hiyo ni wale wasiofuatilia mienendo ya watoto wao shuleni ikiwamo kukagua madaftari. Amkeni mnaosinzia, ili kujiridhisha kama kweli wanasoma.

Katika mazingira hayo, ni rahisi watoto kuwa huru kufanya lolote kutokana na Kwamba hakuna wa kuwafuatilia, matokeo yake ni kujiingiza katika wizi kama huo wa mwanafunzi aliyekamatwa usiku wa manane.

Hivyo, watoto wasipofuatiliwa mienendo yao shuleni inaweza kuwa ni nafasi nzuri kushawishika kirahisi na kuingia katika makundi yasiyofaa na hata kuhatarisha maisha yao.

Ufuatiliaji wa mienendo yao waendapo shuleni ikiwamo na mahudhurio na masomo darasani, utawafanya wawe makini, lakini wakiwa huru kupita kiasi, ni hatari.

Lakini ufuatiliaji huo utakuwa na maana iwapo utakuwa na ushirikiano mzuri kati ya wazazi na walimu, vinginevyo unaweza usizae matunda.

Ninaeleza hivyo, kwa sababu wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawako tayari kuambiwa makosa ya watoto wao, badala yake wanalaumu walimu na hata wakati mwingine kuwatishia usalama wao.

Wazazi na walezi wa aina hiyo wanachangia kuharibu watoto wao kwa kuwakingia kifua hata wanapofanya mabaya, kitendo huwafanya walimu wawaache hata kama watawaona wanajihusisha na vitendo viovu.

Ikumbukwe kuwa, walimu ndio wanaokaa na wanafunzi kwa muda mrefu, ni vyema wakasikilizwa iwapo wana jambo kuhusu tabia za wanafunzi, lakini wakikataliwa, wanakata tamaa na kuacha watoto waharibikiwe na mwishowe wafukuzwe shule.

Mwanafunzi asiye na tabia njema anaweza kurekebishwa kwa ushirikiano mzuri kati ya wazazi na walimu kwa upande kutimiza wajibu wake bila kutegeana.

Hivyo, ingependeza kama wazazi na walezi watasaidia kuimarisha

mahudhurio ya watoto wao shuleni kwa kuwafutilia kwa karibu wakiwauliza walimu ili kujua kinachoendelea.

Kwa njia hiyo ya ushirikiano, mzazi na mlezi atajua kila kitu kuhusu mtoto wake, kwani wapo wale wakiwa nyumbani ni wema, lakini wakishafika mazingira mengine, tabia inabadilika.

Ili kujiridhisha, mtoto anaporudi nyumbani, mzazi afuatilie mwenendo wa masomo yake, ajiridhishe kama kweli anasoma. Ninaamini itakuwa rahisi kujua kila hatua na maendeleo ya mtoto, kwani akiachwa bila kufuatiliwa anakuwa huru hadi kujiingiza katika makundi yasiyofaa.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi, walimu wapewa elimu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa elimu ya fedha na umuhimu wa uwekaji akiba kwa wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Pugu iliyopo Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo inalenga kutoa fursa kwa wanafunzi hao kujifunza masuala ya kifedha ili kuwajengea utamaduni wa kujiwekea akiba, kubuni mawazo ya biashara sambamba na kutambua namna ya kutumia taasisi za kifedha, zikiwamo benki hiyo ili kujinufaisha kiuchumi.

Semina kuhusu mafunzo hayo ilifanyika mwishoni mwa wiki shuleni huko ikiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Compliance NBC, Sarah Laiser, aliyeambatana na viongozi wengine waandamizi wa benki hiyo akiwamo Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Benki ya NBC pamoja na maofisa wengine waandamizi.

Wenyeji waliongozwa na Mkuu wa Shule hiyo, Boniface Orenda, baadhi ya walimu pamoja na wanafunzi.

Akizungumzia hatua hiyo, Sarah alisema ni muhimu kwa kuwa inalenga kuwajengea ufahamu na ujuzi wa kifedha vijana hao wakiwamo wale wanaotarajia kuhitimu elimu ya sekondari na kujiunga na elimu ya juu na wale watakaojiajiri.

"Elimu ya fedha kwa wanafunzi ni muhimu kwa sababu inawawezesha kuelewa mapema jinsi ya kutunza na kuendesha fedha zao, kubuni na kufuata bajeti na kufanya uamuzi sahihi wa kifedha.

"Zaidi, kuwapo kwetu hapa kunalenga kuwasaidia wanafunzi hawa kutambua umuhimu wa akiba, uwekezaji na matumizi sahihi ya mikopo.

"Tunaamini hawa ndio wajasiriamali, wawekezaji na maofisa wa kesho, hivyo ni vema kuanza kuwaandaa mapema ili wajue namna ya kutumia taasisi za fedha katika kujikwamua," alisema Sarah.

Wakiwa shuleni huko, maofisa wa benki hiyo walipata wasaa wa kutoa mafunzo na kuwasilisha mada mbalimbali kuhusu masuala ya fedha, ujasiriamali na kutoa fursa kwa wanafunzi hao, wakiwamo wale wenye mahitaji maalum, kujibu na kujadili hoja mbalimbali kuhusu mada hizo.

"Pia, tumepata fursa ya kutambulisha huduma zetu mahususi kwa wanafunzi na walimu, zikiwamo akaunti za mwanafunzi na akaunti ya mwalimu zilizobuniwa kulingana na mahitaji ya makundi hayo.

"Pia, tumetoa zawadi mbalimbali, zikiwamo jezi za vilabu vinavyoshiriki Ligi Kuu ya NBC, mipira na zawadi binafsi zilikabidhiwa kwa uongozi wa shule pamoja na wanafunzi mbalimbali," alisema.

Aidha, maofisa hao walishiriki upandaji miti ya matunda na vivuli kwenye viunga vya shule hiyo ili kuacha kumbukumbu pamoja na kuunga mkono jitihada za shule hiyo pamoja na serikali katika utunzaji mazingira.

Akizungumzia umuhimu wa mafunzo hayo, Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Orenda pamoja na kuishukuru Benki ya NBC kwa hatua hiyo, alisema elimu hiyo itasaidia wanafunzi hususani wale wanaotarajia kuhitimu kuwa na elimu ya kujiwekea akiba na kujijenga kijasiriamali hata pale watakaposhindwa kuendelea na elimu ya juu zaidi.

"Kimsingi, ujio wa NBC shuleni hapa umekuwa na tija kubwa si tu kwa wanafunzi, bali pia walimu kwa kuwa huduma zao zinatulenga pia walimu.

"Elimu hii imewanufaisha jumla ya wanafunzi 930 wanaosoma hapa ambapo 139 kati yao ni wenye mahitaji maalum.

"Tunashukuru mafunzo yamekuwa shirikishi kwa wanafunzi wa aina zote, wakiwamo wenye mahitaji maalum na wote wameweza kujibu maswali kwa ufasaha na wamepata zawadi," alisema.

Kwa mujibu wa Mwalimu Orenda, umuhimu wa elimu ya fedha kwa wanafunzi hao utaonekana zaidi pindi wanapohitimu elimu yao ambapo baadhi yao hujiingiza katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, ikiwamo biashara na hata wanaoendelea na elimu ya juu, elimu ya fedha imekuwa inawasaidia katika kufanya uamuzi unaohusu fedha wanazozipata, ikiwamo mikopo ya elimu ya juu na fedha wanazotumiwa na wazazi pamoja na walezi wao wakiwa vyuoni.



Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, Rebeka Gyumi, akifungua mafunzo ya kujiamini kwa wasichana 20 yatakayoendeshwa kwa miaka miwili, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali, wadau mazingira kujadili fursa biashara kaboni, taka mijini

**Na Romana Mallya**

WADAU wa mazingira zaidi ya 1,000 kutoka wizara, taasisi, mashirika ya umma, sekta binafsi na vyuo vya elimu ya juu wanatarajiwa kukutana kujadili fursa zilizoko katika hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Fursa hizo ni pamoja na biashara ya kaboni, usimamizi wa taka, mabadiliko ya tabianchi, nishati safi ya kupikia, upandaji miti na usimamizi na uzingatiaji sheria nchini.

Kadhalika, wadau hao wataweka mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto za mazingira nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo jana wakati anazungumzia maandalizi ya mkutano huo wa viongozi, wataalamu na wadau kuhusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi utakaofanyika jijini Dodoma kwa siku mbili kuanzia Septemba 9, mwaka huu.

Alisema viongozi watakaoshiriki ni mawaziri na makatibu wakuu kutoka wizara za kisekta, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri zote Tanzania Bara.

Waziri Dk. Kijaji alisema mkutano huo pia utashirikisha wakurugenzi kutoka katika mashirika ya umma na wataalamu kutoka sekta binafsi na asasi zisizo za kiserikali.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusimamia na kutoa mwongozo mahsusi katika kuhakikisha mazingira na maliasili zinahifadhiwa na kuongeza mchango katika Pato la Taifa.

Alisema mazingira na maliasili ni msingi wa uhai, hivyo usimamizi na hifadhi ya rasilimali hizo ni suala la kipaumbele na lenye umuhimu wa kipekee.

Waziri Dk. Kijaji alisema nchi inakabiliwa na changamoto mbalimbali za mazingira ambazo zinafifisha ustawi wa jamii na uchumi.

"Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa ardhi, uharibifu wa vyanzo vya maji, ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu, upotevu wa makazi ya wanyamapori na bayoanuai.

Alitaja athari nyingine ni mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya pwani na baharini.

"Athari zingine ni uharibifu wa ardhi oevu, uchafunzi wa mazingira na kuenea kwa viumbe vamizi.

"Changamoto hizi zinachangiwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu, ikiwamo utegemezi mkubwa wa kuni na mkaa kama chanzo cha nishati, kilimo kisicho endelevu, utupaji taka ovyo na ufugaji usiowiana na maeneo ya malisho," alisema.

Waziri huyo alisema changamoto hizo zinaathiri sekta muhimu ya uchumi kama vile kilimo, nishati, maji, uvuvi, utalii, ustawi wa jamii na viumbe hai.

Alisema kwa kutambua mchango wa wadau katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu mkutano huo.

Alisema maudhui ya mkutano huo ni pamoja na kujadili na kuweka mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto za mazingira nchini.

Waziri huyo alisema mkutano huo pia unalenga kuimarisha uwajibikaji, ufanisi na usimamizi wa hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri Dk. Kijaji alialika wadau wote katika mkutano huo muhimu kwa mustakabali mpana wa nchi.



Mkuu wa Kitengo cha 'Compliance' cha Benki ya NBC, Sarah Laiser, akipanda moja ya mti wa matunda kwenye viunga vya Shule ya Sekondari ya Wavulana Pugu, jijini Dar es Salaam ikiwa ni kumbukumbu ya ziara ya maofisa hao shuleni hapo kwa ajili ya semina fupi ya mafunzo, kuhusu elimu ya fedha na akiba kwa wanafunzi. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Shule hiyo, Boniface Orenda (aliyevaa suti) na maofisa wengine wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIC yasajili miradi ya Sh. tril. 21.7

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimefanikiwa kusajili zaidi ya miradi 240 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni nane (sawa Sh. 21,698,720,000,000) mkoani Iringa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Kituo TIC, Gilead Teri, alipokuwa mkoani humo kuzungumza na wawekezaji.

Aliwaeleza wafanyabiashara hao kuwa Mkoa wa Iringa una fursa nyingi za kiuchumi na unafaa kuwa eneo la kimkakati kwa uwekezaji.

Alisema miradi hiyo iliyosajiliwa na TIC inatarajiwa kutoa ajira kwa zaidi ya watu 28,000 na kituo hicho kitaendelea kuweka mikakati ya kuvutia uwekezaji mkubwa zaidi kwenye mkoa huo.

Teri alisema fursa za uwekezaji mkoani Iringa zinaweza kupatikana katika sekta kuu nne ambazo ni kilimo, viwanda, uchukuzi na utalii.

Alisema sekta ya kilimo inatoa nafasi za kupanua uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao, huku sekta ya viwanda ikitoa mwanya wa kuanzisha viwanda vya kubadilisha malighafi kuwa bidhaa zenye thamani zaidi.

Kuhusu uchukuzi alisema unatoa fursa za kuboresha miundombinu na utalii unatoa nafasi za kukuza maeneo yenye vivutio vya kipekee kama Hifadhi ya Taifa ya Ruaha (RUNAPA), ambayo sasa inachukuliwa kuwa Serengeti mpya kutokana na ongezeko la watalii.

Pia, alizungumzia faida za filamu maarufu iliyochezwa na Rais Samia Suluhu Hassan ya The Royal Tour katika kukuza sekta ya utalii nchini, akieleza kuwa imeongeza watalii wanaotembelea maeneo mbalimbali, ikiwamo Ruaha.

Alisema Royal Tour imesaidia kubainisha vivutio vya utalii vya Tanzania na kuvifanya kuwa maarufu zaidi duniani, hali ambayo inachangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa sekta ya utalii mkoani Iringa na maeneo jirani.

Aidha, alihimiza ushirikiano wa karibu kati ya TIC, wawekezaji na viongozi wa mkoa, ili kuhakikisha kuwa fursa hizo zinaweza kutumika kikamilifu na changamoto zinatatuliwa kwa ufanisi.

Alisema TIC itaendelea kuwa karibu na wawekezaji wa mkoa huo ili kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara yatakayowavutia wawekezaji wengi zaidi kwenda kuwekeza kwenye mkoa huo.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, aliishukuru TIC kwa kuwatembelea wawekezaji wa mkoa huo.

Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kuwapongeza wawekezaji kwa juhudi zao na kuwaeleza kuhusu fursa zinazopatikana na kusikiliza changamoto wanazokumbana nazo katika shughuli zao za uwekezaji.

# Uchaguzi, Dira ya Taifa kutawala Wiki ya AZAKI

**Na Elizabeth Zaya**

UCHAGUZI wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, Uchaguzi Mkuu mwaka kesho na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo, zinatarajiwa kuwa miongoni mwa agenda kubwa katika mijadala kwenye Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI) inayotarajiwa kuanza Septemba 9 hadi 13, mwaka huu.

Wiki hiyo inatarajiwa kufanyika jijini Arusha na kushirikisha zaidi ya wadau 500 kutoa katika asasi hizo, sekta binafsi, serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo. Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), Justice Rutenge, alisema wiki hiyo imebebwa na kaulimbiu: 'Sauti, Dira na Thamani'.

Alisema kaulimbiu hiyo inaendana na wakati uliopo na matukio yanayoendelea nchini ambayo ni pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu, uchaguzi mkuu wa mwakani na uandaaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025-2050.

"Tupo kwenye kipindi muhimu sana kwenye demokrasia yetu kama nchi, kwa sababu mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mtaa, wote mnafahamu, pia mwakani tuna uchaguzi mkuu, lakini la jambo la kipekee sana, mwakani tunatarajia kuzindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, ambayo ni fursa adimu sana inayokuja mara moja kwa muda mrefu.

"Fursa hii kutokana na umuhimu wake hatuna budi sauti za wananchi zikasikika kuchangia maoni yao wenyewe, kwani Dira ya Taifa inapaswa itokane na sauti, mawazo, mitazamo na maoni ya wananchi," alisema Rutenge.

Alisema wiki hiyo pia itakuwa na mijadala mbalimbali inayohusu shughuli za AZAKi nchini, maendeleo ya jamii na ushirikiano baina ya asasi za kiraia, serikali na sekta binafsi.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kimataifa linaloshughulika katika kusaidia na kuwezesha watu wenye ulemavu wa macho nchini (CBM), Nesia Mahenge, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Wiki ya AZAKi 2024, alisema kuwa kuelekea wiki hiyo maandalizi yamekamilika na kuwashukuru wadau wote waliojitokeza kudhamini na kuwezesha maadhimisho hayo.

Maadhimisho ya Wiki ya AZAKi ni ya sita kufanyika tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018.

# Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuchunguza afya wagonjwa bure

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WANANCHI wa Manispaa ya Morogoro wanatarajiwa kunufaika na upimaji, matibabu na uchunguzi wa kiafya bure kwa magonjwa mbalimbali bure na madaktari bingwa kuanzia Agosti 26-30, mwaka huu katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Morogoro.

Uchunguzi huo ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Meneja wa Shirika la Mzinga ambaye ni Mkuu wa Jeshi Kikosi cha Mazao, Brigedia Jenerali Seif Athumani Hamis, aliwaambia waandishi wa habari kikosini hapo na kuwataka wananchi wa Morogoro na maeneo mengine kujitokeza kwa wingi katika viwanja hivyo kupata huduma hizo za kitabibu, uchunguzi na ushauri wa kiafya bure.

"Tulipewa maelekezo na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda ya kuhakikisha kila eneo tunafanya shughuli mbalimbali za maadhimisho ya miaka 60 ya JWTZ, miaka hii ni mingi sana kwa jeshi, wengine wanafanya mazoezi ya medali, michezo, sanaa, utamaduni na sisi tumeamua kutoa huduma za afya bure kwa wananchi," alisema Brigedia Jenerali Seif.

Alisema huduma hizo zitatolewa na wataalamu wa hospitali ya jeshi hilo ya Mzinga kwa kushirikiana na wataalamu wengine mabingwa kutoka maeneo mbalimbali, ikiwamo majirani zao Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), madaktari wa Manispaa ya Morogoro na wataalamu wengine wabobevu.

Aidha, uchunguzi huo utazinduliwa kesho na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima na kusisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo.

"Katika miaka 60 ya JWTZ tuna mambo mengi ya kujivunia, tumeshiriki ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, mwaka 79 tulimtoa Nduli Iddi Amini, tumewasaidia majirani zetu katika harakati za kujikomboa.

"Hadi sasa askari wetu wako kwenye nchi mbalimbali kuendelea na ulinzi wa amani ikiwamo DRC, lakini tumekuwa tukisaidia huduma za ndani kunapotokea dharura na majanga, tukio la karibuni ni la moto kwenye kituo cha kupokea na kupooza umeme cha Msamvu," alisema.

Kadhalika, alisema bado jeshi hilo liko imara na litaendelea kuhakikisha linalinda amani, mipaka na uhuru wa nchi.

Akizungumzia huduma zitakazotolewa katika siku hizo, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Jeshi Mzinga, Dk. Luteni Kanali Fredrick Maeda, alisema huduma za upimaji, ushauri na tiba zitafanyika kwa magonjwa mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa kansa ya kizazi kwa wanawake, afya ya kinywa na meno, upimaji wa tezi dume, ugonjwa wa kifua kikuu na Ukimwi.

Magonjwa mengine ni pamoja na shinikizo la damu, sukari, ushauri wa mazoezi na tiba.

Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Maneno Focus Matawa, alisema uchunguzi huo ni muhimu wananchi wanapaswa kuchangamkia kutokana na takwimu kuonesha yapo magonjwa mengi, lakini wananchi wameshindwa kupatiwa ufumbuzi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo shinikizo la damu na magonjwa ya kinamama.

"Lakini kupitia zoezi hili, watakuwapo wataalamu wa njia za mkojo, tumegundua kuna changamoto kama za ugonjwa wa UTI kulalamikiwa na wagonjwa kujirudia rudia, wataalamu hawa watasaidia upimaji na ushauri," alisema Dk. Matawa.

Alisema changamoto nyingine ni kwa wagonjwa kulalamikia kuumwa kwa kujirudia kwa magonjwa kama homa ya matumbo (Typhoid) na magonjwa mengine, lakini sababu wakati mwingine hutokana na kununua dawa kwenye maduka na kutumia bila vipimo wala ushauri wa kidaktari ili kupata matibabu sahihi.

"Na hii ni hatari, unaweza fikiri unaugua ugonjwa huu, kumbe labda ni dalili ya ugonjwa mwingine kama saratani n.k, inaendelea kutumia dawa za ugonjwa mwingine kumbe unauacha ule ambao ndio sababu unaendelea kukua, ni vizuri kabla ya kutumia dawa ukapata ushauri na vipimo vya kiuchunguzi," alisema.



## Bosi TANESCO akerwa tabia uchomaji nguzo za umeme

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MENEJA wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Sixmund Mosha, amechukizwa na tabia ya baadhi ya wananchi kuharibu miundombinu inayotumika kuzalisha nishati ya umeme ikiwamo uchomaji wa nguzo.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza juu ya uharibifu uliofanywa na baadhi ya wananchi kwenye miundombinu yao.

Mosha, alisema kutokana na hali ya uchomaji wa nguzo za TANESCO, maeneo ya Kijiji cha Lorbene Kata ya Naberera, walibaini hasara hiyo kwa kuwa haikuwapo huduma ya nishati ya umeme.

"Siku za hivi karibuni kumezuka mtindo wa uharibifu wa miundombinu inayosababishwa na moto inayowashwa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Simanjiro," alisema.

Hivyo, aliwaomba viongozi wa serikali za vijiji, taasisi za kidini ikiwamo misikiti, makanisa na wanaohusika kutoa ujumbe kwa jamii kuwaeleza wasifanye vitendo hivyo.

Alisema: "Ikumbukwe kwamba miundombinu hii ni ghali na ina changamoto za kuirejesha, tuwajibike sote kutoa elimu, kuwakanya na kukemea vitendo hivyo visivyofaa katika jamii."

Aidha, alisema kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzake ili kupiga vita uchomaji moto holela unaosababisha kuunguza miundombinu.

Mkazi wa wilayani humo, Emmanuel Mollel, alisema baadhi ya watu wanaosafisha mashamba mapya ndio wanasababisha hali hiyo kwa kuchoma moto maeneo bila kuchukua tahadhari.

Alisema: "Watu hao, wanapochoma moto maeneo hayo wanashindwa kuzima na kusababisha kuungua kwa mashamba ya majirani na miundombinu ya TANESCO na kusababisha hasara kubwa."

Pia alisema endapo watu hao wakichukuliwa hatua ikiwamo kulipishwa hasara waliyosababisha itawapa funzo kwa ajili ya kuchukua tahadhari.

Mkazi mwingine, Elizabeth Lengenyi, alisema wananchi inapaswa kuwa makini na uchomaji moto holela kwenye mashamba ili kuepusha kuungua kwa miundombinu hiyo.

Kadhalika, alisema mtu mmoja anaweza kusababisha watu wengi kupata hasara kutokana na nishati ya umeme kutokuwapo, vilevile taifa kwa ujumla kununua vifaa vipya vya umeme.

# Jafo: Tuvilinde viwanda vyetu, tununue bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** KILIMANJARO

WATANZANIA wametakiwa kuvilinda viwanda vya ndani kwa kununua na kutumia bidhaa zinazotengenezwa na viwanda hivyo ili kuviwezesha kuendelea na uzalishaji.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, alipotembelea viwanda mkoani Kilimanjaro na kuzungumza na wafanyabiashara pamoja na maofisa biashara mkoani humo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ajira, pato la taifa pamoja na kukuza uchumi kwa ujumla.

Katika ziara hiyo, Jafo alijionea shughuli za uzalishaji, kusikiliza changamoto na kutafuta njia bora ya kuzitatua kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali.

Hivyo, aliwataka Watanzania kuvilinda viwanda kwa kufanya kazi kwa uadilifu, weledi, uzalendo na hofu ya Mungu kwa lengo la kuepuka kusababisha uharibifu unaoweza kutokea, kwa kuwa fedha nyingi zimewekezwa ili kuvifufua na kuviendesha viwanda hivyo.

Pia, alitembelea kiwanda cha kutengeneza vinywaji baridi cha A One Product and Bottles Ltd, Kiwanda cha Bonite Bottlers Ltd, kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro, kiwanda cha kutengeneza vipuri na mitambo mbalimbali cha KMTC.

Vilevile, alitembelea eneo la uwekezaji la bustani ya wanyamapori ya Serval (Serval Wildlife), pamoja na Kiwanda cha Sukari Moshi cha TPC.

Akiwa katika eneo la uwekezaji la bustani ya wanyamapori Dk. Jafo, aliwahimiza Watanzania kutumia muda wao wa mapumziko kufanya utalii wa ndani kwa ajili ya kukuza biashara ya utalii na kuvutia wafanyabiashara katika sekta hiyo na kukuza biashara.

Akizungumza na wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda wa Mkoa wa Kilimanjaro, aliwataka watumishi wa umma kuwasaidia wafanyabiashara, kuwapa ushirikiano na taasisi nyingine za kisekta kutatua changamoto zinazowakabili.

Kadhalika, alihamasisha utekelezaji wa mpango wa viwanda Tanzania, unaoelekeza kuwa kila mkoa unapaswa kuanzisha viwanda vikubwa vitatu, viwanda vya kati vitano na viwanda vidogo 20 kwa ajili ya kukukuza sekta ya viwanda, kuongeza ajira na pato la taifa.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Raymod Mwangala, alisema mkoa huo utaendelea kufufua viwanda vya zamani pamoja na kuanzisha vipya ili kuongeza ajira kwa wananchi.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, akizungumza juzi na wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Sunflag, wakati wa ziara yake ya kikazi katika Mkoa wa Arusha, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# INEC kuandikisha wapigakura wapya 5,586,433

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imesema inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 5,586,433 sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 walioandikishwa mwaka 2019/2020.

Pia imesema baada ya uboreshaji wa Daftari la Wapigakura linatarajiwa kuwa na wapigakura 34,746,638 wenye sifa.

Hayo yalisemwa jana na mwakilishi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi, Givness Aswile, wakati akizungumza katika mkutano wa INEC na wadau wa uchaguzi mkoani hapa.

Alisema kwa Mkoa wa Manyara INEC inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 157,958 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17 ya wapigakura 883,431 waliopo kwenye Daftari la Wapigakura.

Alisema: "Tume inatarajia baada ya uandikishaji Mkoa wa Manyara, utakuwa na wapigakura 1,041,389".

Alisema wapigakura 594,494, wanatarajiwa kuondolewa kwenye daftari la kudumu la wapigakura kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari.

Hata hivyo, alisema hakuna uchaguzi bila vyama vya siasa au hakuna uchaguzi bila kuwa na wapigakura, hivyo aliwaomba wadau kuhamasisha zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.


Alisema suala la mpigakura halina itikadi za kisiasa au za kidini ila viongozi wa dini, siasa na wa asasi za kiraia wanaweza kutoa elimu juu ya kwenda kujiandikisha kwa kuwahamasisha wananchi.

Vilevile, alisema uandikishaji kwa mkoa huo kwa wilaya za Babati, Hanang' na Mbulu, litaanza Septemba 4 hadi Septemba 10 na kwa Wilaya za Simanjiro na Kiteto zitashiriki zoezi likifika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Mjumbe wa INEC, Jaji Asina Omari, alisema kujiandikisha zaidi ya mara moja ni kosa la kisheria.

Alisema: "Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 ambacho kinasema mtu yeyote atakayeomba kuandikishwa zaidi ya mara moja atakuwa ametenda kosa la kisheria".

Alisema mtu anayetenda kosa hilo akikamatwa adhabu yake ni faini isiyopungua Sh.100,000 na isiyozidi Sh. 300,000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita gerezani kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.



# Zahanati yatumia tochi ya mlinzi kuhudumia wagonjwa

**Na Shaban Njia,** NGARA

WAHUDUMU wa afya katika Zahanati ya Rwakaremera Kata ya Kasulo Halmashauri na Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, wanalazimika kutumia tochi ya mlinzi kuwahudumia wagonjwa wakiwemo wajawazito nyakati za usiku, kutokana na zahanati hiyo kutokuwa na huduma ya umeme.

Kero hiyo imeibuliwa juzi na wananchi wa kata hiyo akiwemo, Christina Julius wakati wa ziara ya Diwani wa Kata ya Kasulo, Yusuf Katura.

Ziara hiyo ililenga kusikiliza kero zinazowakabili, wakisema zahanati hiyo waliijenga kwa ajili ya kuwanusuru wajawazito kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 30 kufuata huduma katika Hospitali ya Nyamiaga.

Alisema zahanatihiyo haina nishati ya umeme hali inayosababisha huduma kutolewa katika mazingira magumu nyakati za usiku.

Alisema wagonjwa wakihudumiwa kwa kutumia simu zao za mkononi au tochi ya mlinzi, hivyo kumtaka diwani huyo kuhakikisha anafikisha kilio chao wilayani ili umeme upatikane.

**Alisema zahanato hiyo haina nishati ya umeme hali inayosababisha huduma kutolewa katika mazingira magumu nyakati za usiku.**

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Jonathan Zofilo alisema kukosekana kwa huduma hiyo ni kikwazo kwa watoa huduma na wagonjwa wanaotafuta matibabu nyakati za usiku hasa kwa wajawazito na watoto, kwamba lisipotatuliwa kwa haraka wengi wanajifungulia gizani na kupoteza maisha.

Mlinzi wa zahanati hiyo, John Nkwale alisema, imekuwa ikitumika tochi yake katika kuwahudumia wagonjwa, hali aliyoitaja kuwa kikwazo kwa wagonjwa na wakati mwingine wanalazimika kwenda hospitalini kuepuka usumbufu.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, John Samweli alikiri zahanati hiyo kutokuwa na umeme na kuwa mara nyingi wamekuwa wakitoa huduma mchana pekee na mara chache sana nyakati za usiku.

Diwani wa Kaya ya Kasulo, Yusuf Katura alisema, kilio cha kukosena kwa nishati ya umeme katika zahanati alishakifikisha na kulisemea katika baraza la madiwani ili kuangalia namna ya kulitatua.



Maofisa kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina wakiangalia shughuli za uzalishaji walipotembelea shamba la kilimo biashara linalofadhiliwa na mgodi wa Barrick North Mara wakati wa ziara yao ya kutembelea migodi ya Twiga na Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi za umma zenye madeni kukatiwa huduma ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson, ameuagiza uongozi wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kukata huduma ya maji kwenye taasisi za umma ambazo zina madeni ya muda mrefu.

Alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa mwaka wa wadau wa maji wilayani hapa, kuzitaka taasisi hizo za umma zisizolipia huduma kushughulikiwa kama ilivyo kwa taasisi nyingine.

Alisema: "Nawashagaa RUWASA mnalia na madeni ya bili za maji kwenye taasisi za umma, zinapaswa kushughulikiwa kama taasisi zingine. Kateni huduma ya maji kwao, na kama kuna taasisi pia ya serikali ambayo inadaiwa bili za maji, natoa mwezi mmoja ilipe deni hilo vinginevyo nitachukua hatua".

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude licha ya kuupongeza wakala huo aliagiza kuhakikisha ifikapo Desemba mwaka huu, miradi yote ambayo wanaitekeleza iwe imekamilika na kuhudumia wananchi.

Meneja wa RUWASA Wilaya, Dickson Kamazima, alisema kipaumbele chao ni kuyafikia maeneo yote ambayo hayana huduma ya maji pamoja na kuikamilisha miradi ya maji kwa wakati ambayo inatekelezwa ili kuwaondolea adha wananchi kutumia maji yasiyofaa kiafya.

Alisema licha ya kuendelea kutoa huduma stahiki za maji wanakabiliwa na tatizo la baadhi ya taasisi za umma kutolipa bili za maji kwa wakati, hivyo kuwapa wakati mgumu katika uendeshaji na matengenezo ya miundombinu.

## DC apiga 'Stop' mawakala kulipa ushuru wa barabara

**Na Judith Julius,** NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Julius, ameagiza kusitishwa kwa shughuli za vijana 'mawakala' kulipia ushuru wa barabara kwa niaba ya madereva wa malori katika eneo la Kabanga OSBP wilayani humo.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya katika eneo hilo, kutatua mgogoro uliohusisha vijana waliokuwa wanafanya kazi ya kulipa ushuru wa barabara kwa niaba ya madereva wa magari makubwa ya mizigo toka Burundi kuingia Tanzania.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya kuhusu mawakala hao na mgogoro uliokuwepo, Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika eneo hilo, Laurent Kagwebe alisema vijana hao toka pande Burundi na Tanzania, walikuwa wanafanya kazi ya kulipia ushuru wa barabara kama mawakala wa madereva wa magari makubwa ya mizigo kwa makubaliano kati yao na madereva wa magari hayo.

Kagwebe alidai kuwa kazi hiyo ilikuwa inafanyika kinyume na sheria za forodha na kuwa walivyoelezwa waliona wanadhulumiwa haki ya kupata riziki, hivyo kuomba kukutana na Mkuu wa Wilaya ya Ngara kwa maelekezo zaidi.

Baada ya kuwasikiliza vijana hao Mkuu wa Wilaya, Julius aliagiza kusitishwa kwa shughuli hizo mpaka pale utaratibu mwingine ulio bora na usiyokinzana na sheria za forodha zilizopo katika kutekeleza majukumu ya TRA, utakapoandaliwa.

Kufuatia agizo hilo vijana hao waliahidi kuwa watulivu na kufuata maelekezo hayo wakati suala lao linaendelea kufanyiwa kazi.

## Wataka serikali, viongozi wa dini kudhibiti mauaji

**Na Daniel Limbe,** KARAGWE

WADAU wa maendeleo wameiomba serikali kukutana na wadau mbalimbali wa maendeleo, viongozi wa dini kujadilili namna ya kudhibiti matukio ya mauaji nchini pamoja na watu kujiua.


Ombi hilo lilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Mavuno Project, Charles Bahati wakati wa maadhimisho ya miaka 30 ya utendaji kazi wa shirika hilo pamoja na mahafali ya sita ya kidato cha nne kwa wanafunzi wa Sekondari ya Mavuno model.

Bahati alisema kuongezeka kwa vitendo vya mauaji na kujiua inaonyesha kuwepo kwa udhaifu mahali, kwamba ili kuondoka hali hiyo ipo haja kwa serikali na wadau wa maendeleo kukaa pamoja ili kujadili na kupata ufumbuzi wa mambo hayo.

Alisema vitendo hiyo vinachafua taswira nzuri ya vijiji na wilaya ambako matukio hayo yanatokea jambo linaloweza kudumaza uchumi wa wananchi kutokana na baadhi yao kuishi kwa hofu.


Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa alisema serikali ipo tayari kukutana na wadau mbalimbali wa maendeleo pamoja na viongozi wa dini ili kutafuta mwarobaini wa matukio hilo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 27, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

NDIVYO MKONGO WA TAIFA UNAVYOLETA MAGEUZI TEHAMA



Ukurasa 13

Kutana na kinara teknolojia ya tiba ya kupandikiza viungo



Ukurasa 14

**USHUHUDA WA WAKULIMA: Mbegu za asili za mpunga zinafanya maajabu shambani**

TEKNOLOJIA

**NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO**

SUA YAWAHAKIKISHIA WAKULIMA

# Inawezekana kulima mpunga bila mbolea za viwandani, viuatilifu vya kuulia magugu

MATUMIZI ya mmea azola yanayogunduliwa na wasomi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ni teknolojia mpya ya kuzalisha mpunga mwingi bila mbolea wala dawa ya magugu.

Kimsingi, azola inaua magugu yanayovamia mpunga, pia ni mbolea ya asili hulazimiki kutumia pembejeo za viwandani shambani, yote hayo yakipunguza gharama na kuongeza mazao na kuimarisha ubora wa ardhi, anasema Yerominus Ambrose.

Ambrose, Fundi Sanifu Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia ya Chuo Kikuu cha SUA, anasema hayo wakati wa maonesho ya wakulima Nanenane Kanda ya Mashariki yaliyomalizika mkoani Morogoro.

Anawashauri wakulima wa mpunga kutumia azola katika kukabiliana na magugu shambani ili kuwa na kilimo chenye uhakika hasa kwa mimea inayostawi kwenye maji mengi, mfano mpunga.

Ambrose anasema azola ina uwezo mkubwa kwenye mpunga na kuleta faida zaidi kwa mkulima, akitaja mwaka 2023 walitafiti kwenye maabara na kubaini kuwa ina nitrojeni (kirutubisho) nyingi zaidi ya iliyopo kwenye mbolea za viwandani.

"Inafaa kutumika ni mbadala wa mbolea za viwandani wakulima wengi wa mpunga wanazozitumia," anasema Ambrose.



Azola na mpunga. **PICHA: SUA**

Anaongeza kuwa, azola inachukua naitrojeni kwenye hewa angani na kuiingiza kwenye maji ardhini na kutumiwa na mimea inayokua na kuulinda dhidi ya magugu shambani.

"Mmea huu ukipandwa kwenye mazao yanayohitaji maji mengi inaachilia naitrojeni iingie kwenye mpunga na kuukuza kwa ubora, na kuuhakikishia kuleta tija kwenye mavuno," anasema.

Anasema tayari wameshawafundisha baadhi ya wanachuo wa SUA ambao wameanzisha mradi wa kupanda mmea huo kuwauzia wakulima mbalimbali tena wakilenga kuuza kwenye kampuni na taasisi za kilimo na ufugaji za umma na binafsi.

"SUA inakabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana, itawawezesha kujiajiri kwa kuanzisha mashamba ya azola na kuuza kwa wakulima na wafugaji," anasema Ambrose.

Nyasi hizo hulisha; sungura, ng'ombe na mbuzi na kuongeza faida kwa mfugaji na mkulima ambaye hatalazimika kununua majini au vyakula vingine kwa gharama kubwa.

Mwanafunzi aliyehitimu digrii ya Sayansi ya Wanyama SUA mwaka 2023 na kufanya biashara ya mmea wa azola, Rainfred Malekela, anasema ameanzisha kampuni ya Yoborini Farm kulima azola na kupunguza gharama ya uwekezaji kwenye mifugo kwa wakulima.

Rainfrida anasema ameshatumia njia mbalimbali za mimea kuzalisha kitu chenye kuleta tija katika kilimo na mifugo ikiwemo azola, black sodiam na red arms ambavyo ni gharama nafuu na kuongeza uzalishaji huku ikimpunguzia mkulima au mfugaji gharama za chakula.

Anasema amebaini azola ina nafasi kubwa ya kumkomboa mkulima na mfugaji katika kupunguza gharama za uzalishaji kwa sababu inapunguza tatizo la chakula cha mifugo.

Anawashauri Watanzania kurudi kwenye vitu vya asili kwa kuzalisha bila gharama kubwa, kuachana na sumu za viwandani na kupata faida zaidi badala ya kutumia pembejeo za viwandani ambazo zina gharama kubwa na baadaye huambulia faida kidogo.

Anasema licha ya kuwa, mfanyabiashara wa zao hilo anakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa masoko na uelewa mdogo, ni jambo linaloleta matumaini kama likifahamika zaidi kwa wakulima na wafugaji.

Ana neno kwa wafugaji wa kuku hasa 'Broiler' akiwataka kutumia majani hayo kulisha mifugo kwa sababu yana nafasi ya kuongeza uzito wa kuku kutoka kilo moja wa kuku wa mwezi mmoja na kufikia gramu 1,200 hadi 1,400 ambayo ni sawa na kilogramu 1.2 au 1.5.

"Broiler wanatofautiana bei kutokana na uzito, yupo mwenye kilo moja anayeanzia kuuzwa kwa Shilingi 5,500 na ukizalisha kwa kutumia azola anafikia Sh. 7,500 hadi 8,500 na hivyo kukuletea faida zaidi mfugaji," anasema Reinfreda.

Anawashauri wakulima na wafugaji kutumia azola ili kupunguza gharama za kilimo na chakula kwa ajili ya mifugo huku wakizalisha kwa ubora wanaoukusudia au zaidi.

Pia, wakiachana na uzalishaji wa kutumia gharama kubwa huku wakiambulia faida kiduchu.

TEKNOLOJIA

NA AUGUSTA NJOJI, DODOMA

# HIVI NDIVYO MKONGO WA TAIFA UNAVYOLETA MAGEUZI TEHAMA

UJENZI wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni miongoni mwa miundombinu ya habari na mawasiliano yanayowezesha Tanzania kushiriki uchumi wa kidijitali, unaochochewa na matumizi ya TEHAMA.

Mwaka 2009, serikali inatangaza dhamira ya kujengwa mkongo huu katika mizunguko mikuu mitatu ya kaskazini, kusini na magharibi na kisha kujengewa njia nyingi mbadala ili kuwa na mawasiliano ya uhakika.

Lengo ni Tanzania kuwa kitovu cha huduma za TEHAMA kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 iliyohuisha mwaka 2016.

Mkurugenzi wa Miundombinu ya TEHAMA wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Leo Magomba, anaeleza namna mkongo ulivyofanikisha mageuzi ya TEHAMA.

Anasema umewezesha kuwapo mawasiliano ya mtandao yanayosafiri kwa kasi, yenye ubora wa hali ya juu na uhakika yanayosafiri kwa kasi ya mwanga.

Anafafanua kuwa mkongo huo unasafirisha mawasiliano kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na teknolojia nyingine zilizopo kama waya wa shaba, satellite, mawimbi na redio.


"Mkongo wa mawasiliano ni moja ya miundombinu ya msingi kama ilivyo mingine mfano barabara, maji, umeme na gesi, mkongo una uwezo mkubwa wa kubeba na kusafirisha mawasiliano kwa kasi zaidi ya kilometa 300,000 kwa sekunde," anasema.

Uwezo huo ni suluhisho la kupatikana mahitaji ya sasa na ya baadaye ya matumizi ya intaneti, biashara za elektroniki, tiba na elimu mtandao.

Magomba anasema mkongo huo umetengenezwa kwa nyuzi za kigae ndogondogo zinazotokana na vioo vilivyoyeyushwa na hatimaye kutengenezwa nyuzi nyembamba kwa ajili ya kusafirisha mawimbi ya mawasiliano kwa kasi ya mwanga.

Kuongezeka kwa matumizi ya nyaya hizi za kigae kumetokana na kukua kwa teknolojia kulikosababishwa na mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo yanajengwa na mkusanyiko wa matumizi mbalimbali ya kidijitali na teknolojia za kisasa kama vile sayansi ya data, ndege bila rubani, roboti, akili mnemba pamoja na kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa matumizi ya TEHAMA.

"Kuna kuongezeka kwa kasi kwa matumizi ya serikali, elimu, afya, mikutano na biashara mtandao pamoja na mitandao ya kijamii ikiwamo youtube, facebook, whatsapp, instagram na twitter (kwa sasa x)," anasema.



Mkongo wa Taifa unavyoonekana. **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kuwa mkongo unaunganisha mikoa, wilaya na vituo vya mipakani vya Tanzania, watoa huduma za mawasiliano ndani ya nchi na pia kusafirisha watoa huduma wa nje ya nchi kwenda kuwaunganisha na mikongo ya baharini au watoa huduma wa nchi jirani.

Anasema hadi sasa mkongo umeunganisha makao makuu ya mikoa yote, wilaya 99, mataifa ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi na Mikongo ya Baharini ya SEACOM, EASSY na 2AFRIKA inayopatikana nchini.

Anaongeza kuwa mkongo unatoa mawasiliano kwa nchi zisizopakana na bahari na mataifa jirani yanayopakana na Tanzania na lengo ni kuongeza kasi na uaminifu wa intaneti, na pia kufikia maeneo ambayo hayajaunganishwa na intaneti kwa sasa.

### GHARAMA NAFUU

Magomba anasema umewezesha watoa huduma kufikisha mawasiliano kwa wateja kwa haraka na uhakika kwa unafuu na hivyo kuharakisha maendeleo kupitia fursa mbalimbali zinazotumia TEHAMA.

"Faida ya mkongo wa taifa wa mawasiliano unawezesha usafirishaji wa data kwa haraka, taarifa kwa kasi na ubora wa hali ya juu na kuleta maendeleo katika sekta ya habari na mawasiliano, pia uwezo na ubora mkubwa unaoruhusu watoa huduma wote kuutumia bila upendeleo, kumeleta faida nyingi nchini."

"Hii pia imepunguza gharama za uwekezaji kwa watoa huduma za mawasiliano na kujengwa kwa mkongo mmoja wa kitaifa kunapunguza gharama za kila mtoa huduma," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema mkongo huo umeharakisha maendeleo ya kiuchumi nchini hata mahali ambapo kampuni za simu hazikuona faida kibiashara.

"Gharama zimekuwa nafuu za mawasiliano kwa wananchi; kuongezeka kwa upatikanaji na ubora wa huduma za mawasiliano, hii inatokana na uwepo wa Mkongo huu unaoruhusu upitishaji wa mawasiliano yenye kasi na kiasi kikubwa," anasema.

### ONGEZEKO LA MATUMIZI

Anabainisha kuwa ukuaji wa sekta unaonekana kwenye ongezeko la matumizi ya simu za mkononi, intaneti, miamala ya kifedha na ongezeko la mifumo mbalimbali ya kutolea huduma kwa njia ya mtandao.

Kwa mujibu wa taarifa inayotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) mwaka 2010 kulikuwa na laini za simu milioni 20.8 na hadi Juni mwaka huu zilifikia milioni 76.6 huku idadi ya laini za intaneti ikiongezeka na kufikia milioni 39.3 kutoka chini ya 500,000.

Magomba anasema mkongo ni chanzo cha mapato ya moja kwa moja ambapo fedha zinatokana na mauzo ya huduma zinazotokana na mawasiliano ya nje na ndani ya nchi.

"Mkongo umezalisha ajira kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo vituo vya kutoa huduma za intaneti, uwakala wa huduma za kifedha kwenye mitandao ya simu, kufanya biashara mitandao, ubunifu wa mifumo na ajira rasmi kwenye kampuni za mawasiliano na serikalini," anasema.

### MWAKA 2024/25

Katika bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2024/25 iliyopitishwa na bunge, inakusudia kutumia takribani Sh. bilioni 80 kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Miongoni mwa shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi huu ni kutengeneza mfumo wa kitaifa wa miundombinu ya mawasiliano ya TEHAMA kijiografia, kuwezesha usanifu wa ujenzi wa kituo cha kitaifa cha kuhifadhi data Dodoma na Zanzibar.

Aidha, kuendeleza na kutekeleza uunganishwaji wa miundombinu ya mkongo wa mwisho kwa taasisi 100 za haki jinai, ulinzi na usalama (mahakama, TAKUKURU, polisi, magereza, jeshi la ulinzi, usalama).

Vituo vya afya na shule kwenye mikongo ya mwisho na uunganishaji wa wilaya 40 kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Nyingine ni kuwezesha uboreshaji wa vifaa vya mikutano ya video katika wilaya 100, ujenzi wa kilomita 186 za mkongo kutoka Kigoma hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; kujenga 'Wi-Fi' katika maeneo 50 ya umma.


Mengine ni kufanya upembuzi yakinifu wa programu ya kitaifa ya ukuzaji wa miundombinu ya kidijitali; kufanya ufuatiliaji wa miundombinu ya 'broadband' na kusimamia ujenzi wa kituo TEHAMA mji wa serikali Mtumba.

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Kutana na kinara teknolojia ya tiba ya kupandikiza viungo

• Alianza kujaribu mbwa akimbandika vichwa viwili



Maini na figo ni viungo vinavyoweza kupandikizwa ili kuokoa maisha. **PICHA: MTANDAO**

MIAKA 55 iliyopita daktari wa Urusi Vladimir Demikhov, anaanza kutimiza ndoto ya kupandikiza tishu na viungo vya binadamu, bila kujua kuwa amefungua njia ya tiba inayookoa maelfu leo.

Anamwalika mpigapicha wa Jarida la LIFE, kumpiga picha akiwa na msaidizi wake, Dk. Vladimir Goriainov, wakifanya upasuaji wa mwisho wa kuunda mbwa mwenye vichwa viwili, yaani akipandikizwa kichwa kingine.

Demikhov alielezea kuwa mbwa mwenye miaka tisa angetumika kupandikizwa vichwa hivyo na mwingine mdogo, ambaye kichwa chake kitachokatwa na kupandikizwa kwa mbwa mkubwa.

Makala iliyochapishwa na Moscow, ikiandikwa na Edimund Stevens, ililelezea kwa undani upasuaji wa saa tatu na nusu.

"Kwanza, walichanja chale chini ya shingo ya mbwa mkubwa na kupata mshipa wa shingo, mishipa ya damu na sehemu ya uti wa mgongo na ya fahamu.

Mwili wenye kichwa na miguu wa mbwa mdogo uliwekwa kwenye meza ya upasuaji karibu na mbwa mkubwa.

Na wawili hao wakafanya operesheni na kisha wakashona. Na upasuaji ukaisha."

Picha za rangi nyeusi na nyeupe, ambazo zilionekana katika toleo la Julai 1959 la gazeti la LIFE, zilionyesha operesheni hiyo.

Hata hivyo kiumbe huyo mwenye vichwa viwili aliishi kwa siku nne.

Hakuwa mbwa wa kwanza wa Dk. Demikhov mwenye vichwa viwili, alikuwa amefanya jaribio hilo mara 23 kwa viwango tofauti vya mafanikio. Moja ya uumbaji wake huo wa vichwa viwili uliishi kwa siku 29 au mwezi.

**ALICHOLENGA**

Wakati akifanyakazi hiyo, bingwa Demikhov aliliambia jarida la LIFE, kuwa lengo la majaribio yake lilikuwa kuonyesha dunia kuwa kupandikiza tishu na viungo vyenye afya ni kunawezekana.

Bingwa huyo wa Urusi, leo ndoto yake imetimia ni ya kupandikiza viungo ni jambo la kawaida, lakini haikuwa rahisi hadi mwishoni mwa miaka ya 1960 ambapo upandikizaji wa ini na moyo ulifanyika kwa mafanikio.

Lakini kwa wale waliosoma makala ya jarida la Life katika miaka ya 1950, maono ya Demikhov juu ya upandikizaji wa vichwa viwili yalionekana kama ya kutisha.

"Tutaanza na benki ya tishu au seli mbalimbali za mwili" daktari wa Soviet alimweleza mwandishi wa gazeti la Moscow.

"Hatimaye itajumuisha kila sehemu ya mwili wa binadamu, jicho, mboni za macho, maini, figo, mioyo na hata miguu.

"Kila kitu kitawekwa kwenye friji. Tutakapokuwa tayari, mwathirika wa ajali ataletwa na jeraha baya. Na tutampatia kiungo muhimu kutoka katika benki yetu. Ikiwa upandikizaji utafanikiwa, ataishi. Ikiwa haujafanikiwa, tutafanyia mwingine."

**KUKOSOLEWA**

Baadhi ya matabibu walimkosoa, mmojawapo ni huyu, anayesema:

"Napata hisia mchanganyiko ninapoona picha hizo kwa sababu ni wanyama ambao, kwa maneno rahisi, waliteswa," anasema Igor Konstantinov.

Ni daktari maarufu wa kimataifa wa upasuaji wa moyo na mishipa ambaye alihitimu huko St. Petersburg na kufanya kazi katika Hospitali ya Watoto ya Royal huko Melbourne, Australia.

Demikhov aliyezaliwa 1916 kutoka familia masikini, baba yake alikufa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Urusi na mama yake alidhamiria watoto wake watatu wapate elimu nzuri.

Alisoma baiolojia katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Moscow, na kuhitimu kwa daraja la juu mwaka 1940.

Miaka 20 mbele, ndipo alipoanza majaribio kuhusu upandikizaji wa viungo na tishu. Mbali na mbwa wake wenye vichwa viwili, alifanya tafiti nyingine pia. Mwaka1937, Demikhov aliunda kifaa cha kwanza cha kusaidia moyo.

Mapema 1946, alifanya upandikizaji wa vingo vya ndani ya mwili kwa wanyama, ukiwamo moyo na mapafu.

Ni majaribio ya kwanza kufanikiwa ya upandikizaji kwa wanyama. Pia alifanya operesheni ya kwanza ya mishipa ya kusukuma damu moyoni na upandikizaji wa kwanza wa ini, miongoni mwa mambo mengine.

> "Kwanza, walichanja chale chini ya shingo ya mbwa mkubwa na kupata mshipa wa shingo, mishipa ya damu na sehemu ya uti wa mgongo na ya fahamu.

"Ni ngumu sana kuelewa ni kwanini, alikuwa na msukumo huu wa ajabu wa kupandikiza viungo," anasema Konstantinov.

"Ninaweza kukisia kwamba alitaka kufanya jambo kubwa kwa nchi yake na kwa manufaa ya ubinadamu. Nadhani, hili ndilo jambo ambalo lilikuwa muhimu kwake."

**MCHANGO UNAOKUMBUKWA**

Mchango wa Demikhov katika upandikizaji ni mkubwa mno. Dk Christian Barnard, aliyefanya kazi ya kwanza ya kupandikiza moyo wa mwanadamu duniani, alimwita "baba wa upandikizaji wa moyo na mapafu."

Lakini mbwa wake wenye vichwa viwili waliharibu sifa yake hasa katika nchi yake.

"Maofisa walimtangaza kuwa mzushi, na majaribio yake yalipigwa marufuku," anasema Konstantinov. "Alilazimika kufanya kazi katika Idara ya Upasuaji ambayo iliongozwa na Alexander Vishnevsky, daktari mkuu wa upasuaji wa jeshi la Soviet."Kwa hivyo alilindwa na jeshi la Urusi ili aweze kuendelea na majaribio yake.

"Lakini naweza kukuambia kama mwanafunzi wa matibabu katika Umoja wa Kisovieti na kisha Urusi, sikuwahi kusikia juu ya Demikhov. Jina lake halikutajwa," anasema mtaalamu huyo ambaye alihitimu katika Chuo cha Tiba cha Kijeshi Saint Petersburg, Urusi mwaka 1992.

Lakini katika maeneo mengine, mafanikio yake yanapendwa.

"Anastahili sifa miongoni mwa madaktari bingwa wa majaribio ya upasuaji na kupandikiza viungo. Hajatambulika kama inavyotakiwa," liliandika jarida la The Annals of Thoracic Surgery mwaka wa 1994.

Katika mwaka wa kifo chake, alitambuliwa nchini Urusi na akapewa heshima ya juu. Dk. Demikhov alikufa akiwa na umri wa miaka 82 mwaka 1998 katika nyumba yake nje kidogo ya Moscow.

"Kila kitu alichofanya kilikuwa kwa manufaa ya wagonjwa duniani kote, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, wamefaidika na majaribio yake," anasema Konstantinov.

"Jambo la muhimu zaidi, aliweza kuwashawishi watu waliomfuata kwamba jambo lisilowezekana linawezekana."

**BBC SWAHILI**

SAYANSI

NA CHRISTINA MWAKANGALE

USHUHUDA WA WAKULIMA

# Mbegu za asili za mpunga zinafanya maajabu shambani

WATETEZI wa mbegu za asili mara zote wanakosoa zile za kisasa zikiwamo zilizoboreshwa kwa teknolojia ya uhandisi jeni (GMOs), wakisisitiza kuwa zina athari kwa binadamu.

Katika Halmashauri ya Shinyanga, matumizi ya mbegu za mpunga za asili, yamethibitisha kuwa zina ubora, baada ya kubadilisha maisha ya wakulima wanaozalisha na kuwapatia faida, bila kuhofia athari za mabadiliko ya tabianchi.

Athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na ukame, mvua hafifu, upepo, wadudu waharibifu na mafuriko.

Kwa mujibu wa Shirika la Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi ya Kiikolojia (PELUM), mkoani Shinyanga, msimu wa mvua eneo hilo unaanza Oktoba hadi Mei, huku Desemba ikiwa na kiwango kikubwa zaidi na wastani wa kati ya milimita za ujazo 450 hadi 990 kwa mwaka, kiwango kinachofaa kwa mpunga.

Pamoja na mpunga, maharage, alizeti na pamba ni mazao yanayozalishwa kwa mujibu wa Ofisa Programu kutoka PELUM, Pessa Kussaga.

Anasema mpunga unaotumika kwa chakula na pia kibiashara, ingawa mbegu zisizo bora ilikuwa changamoto.

Ofisa Programu wa PELUM Kussaga, anazungumza na Nipashe akieleza kuwa utafiti na mfumo wa mbegu za asili umefanikisha kupunguza umaskini uliokithiri kwa baadhi ya wakazi wa halmashauri hiyo.

Anasema Mfumo wa Mbegu Unaosimamiwa na Mkulima (FMSS), ni utaratibu unaowezesha mkulima kutumia na kutunza mbegu za asili na kuzipanda katika msimu ujao, akizitunza kwa njia ya asili bila kuziwekea kemikali.

Kussaga anasema mfumu huo, ulikuwa hatarini kutoweka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Na kwamba ni mfumo unaolinda mbegu za asili kutunza ikolojia.

Kwa upande mwingine ni mfumo wa kilimo hai ambao unahamasishwa na shirika hilo kwa manufaa ya mazingira, kilimo endelevu, kwa kutumia mbolea na mbegu asili.

Anasema wapo baadhi ya wakulima ambao wamenufaika na FMSS kwenye mradi huo, ambao wanauza na kutumia mbegu aina hiyo ambazo sasa zinachangamkiwa na wakulima wengi eneo hilo ni Veronica Richard (40), mwenye watoto wanne.

Veronica, amejiunga na kikundi cha wakulima kikundi cha Songambele, chenye wanachama 26, kati yao wanawake 21, wakazi wa kijiji cha Ichongo, Iselamagazi.

Mwingine ni Emmanuel Sali (52), baba wa watoto watano, akisomesha wengine chuo kikuu, sekondari na wawili shule ya msingi.

Emmanuel ni mwanachama wa Kilimo Hifadhi kikundi chenye wanachama 20 wakiwamo 16 wanawake na wanaume wanne, anaishi kijijini Mwamakaranga, Iselamagazi.

Pessa anasema Shirika la Maendeleo ya Jamii Tanzania (TIDO), lilihusika katika mradi wa kuwaelimisha wakulima ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutumia mbegu za asili ambazo nazo zina ubora.

"Ushirikiano wa TIDO katika kuwezesha jamii kuhusu mbinu za uzalishaji kwa kutumia pembejeo za kilimo zisizo za kemikali, umeimarisha tija na matumizi ya mbegu za kienyeji katika FMSS.

"Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima kuongeza kipato, ulilenga kupunguza umaskini, kuanzisha maonesho ya mbegu za ndani na ushirikishwaji wakulima katika ngazi za vijiji, kata, wilaya na kitaifa kuwasaidia kupata uzoefu na ujasiri wa kueleza kuhusu mbegu za asili na kuzitumia," anasema Pessa.

Anasema utendaji kazi mbegu za asili ni mzuri iwapo zitahifadhiwa ipasavyo bila kemikali, kwa kutumia dawa za asili na unawahakikishia wakulima usalama wa chakula na kuongeza kipato.

**WAINUKA UCHUMI**

Veronica na Emmanuel, ni kati ya wakulima wadogo wa mpunga walioanza kunufaika na kilimo hicho, wanasema kabla ya mwaka 2020, hawakupata mazao yenye tija kutokana na mbegu walizotumia awali.



Mafunzo kwa vitendo ya kilimo bora katika Kijiji cha Mwamakalanga. **PICHA: PELUM**

> "Familia inanufaika kutokana na uzalishaji wa Malamata, sote tunashiriki katika mnyororo wa thamani na tunalipa karo za shule, chakula kilichopatikana na uwekezaji katika chaguzi nyingine za kujikimu".

Kwa sasa wanatumia mbegu za asili za malamata, matela na lugata. Kukosekana mvua za uhakika na mbinu duni za kilimo, kiwango cha uzalishaji kwa aina zote za mbegu ilikuwa mifuko 20 katika ekari mbili, anasema Veronica.

"Kwa jumla, mavuno hayakutosha kukidhi mahitaji ya kaya ya chakula na kuuza ziada kwa mahitaji mengine ya familia zao, ambayo yanahitaji pesa taslimu." Anasema mkulima huyo.

**WAFIKIWA NA TIDO**

Wakulima hao walifikiwa na TIDO kuhamasishwa, kuwezesha jamii kuondokana na umaskini na kuwa na usalama wa chakula.

TIDO ni taasisi isiyo ya kiserikali iliyopo katika halmashauri hiyo kuunga mkono juhudi za serikali, kwa kuwajengea uwezo wakulima wadogo, ili kuwa na kilimo chenye tija na kupambana na umaskini.

Pessa anasema eneo hilo kuliundwa kikundi cha wakulima 30 wa vijiji vya Mwamakalanga, Ichongo, lyabusalu na Bukamba, wakaanza utambuzi wa mbegu za mpunga na mahitaji ya soko kwa kuzingatia ubora.

Anasema wakulima walichagua mbegu zinazoongeza chakula na kipato, malamata ilichaguliwa kuwa mbegu bora zaidi kwa mazingira ya eneo hilo.

Anazungumzia mbegu zilizoboreshwa Pessa anasema kila familia inatumia mbegu ya Malamata na kupunguza ununuzi wa mpunga wa kupanda kila msimu.

Mbegu ya malamata ni ya asili, ambayo inatumiwa na wakulima wa eneo hilo baada ya kupewa elimu namna ya kuitunza na iwapo shambani kwa kuwekewa mbolea ya asili.

"Familia inanufaika kutokana na uzalishaji wa Malamata, sote tunashiriki katika mnyororo wa thamani na tunalipa karo za shule, chakula kilichopatikana na uwekezaji katika chaguzi nyingine za kujikimu".

"Mahitaji ya soko la mchele wa malamata ni makubwa, unaweza kuuza muda wowote kwa bei kubwa ukilinganisha na aina nyingine zilizoboreshwa," anasema Veronica.

Anasema kabla mradi huo mbegu za kienyeji zilikuwa zikimilikiwa na wakulima wachache kijijini hapa, wengi walikuwa wakinunua mbegu za ushirika, lakini hivi sasa karibu kila mmoja anahifadhi yambegu za kienyeji.

Veronica anaongeza kuwa baada ya miaka mitatu ya kilimo hicho, alibaini mabadiliko kutokana na ongezeko la mapato kwa uzalishaji wa mpunga malamata.

Anafurahia kuwa familia yake imenunua ekari 15 za ardhi kwa kupanua eneo la uzalishaji na tano ujenzi wa makazi.

Emmanuel anasema amejenga nyumba ya biashara na ukumbi kama chanzo kingine cha mapato mbali na kilimo, wakati kwa familia ya Veronica kutoka Kijiji cha Ichongo, amezalisha mbegu ya malamata kwa miaka mitatu.

Anasema wamenunua ng'ombe wanne, kujenga nyumba na kusomesha watoto kwa kuuza mbegu hizo na mchele, zinazokubalika na wengi.

Pessa anasema TIDO imechangia ongezeko la uzalishaji wa mpunga kwa ekari kutoka magunia 10 hadi 15.





# NFRA yapiga kipenga ununuzi tani 102,000 za nafaka

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kupitia ofisi zake za kanda ya Sumbawanga mkoani Rukwa imezindua ununuzi wa tani 102,000 za mazao ya nafaka katika msimu wa mwaka 2023/24.

Tani hizo zinajumuisha 90,000 za mahindi na tani 12,000 za mpunga, ambazo ni kiasi cha ziada ya mazao hayo kilichozalishwa na wakulima katika wilaya tatu za Nkasi, Kalambo na Sumbawanga mjini.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu, Meneja wa NFRA Kanda ya Sumbawanga, Marwa Range, alisema msimu wa ununuzi wa nafaka hizo ulizinduliwa katika kanda hiyo Juni 10, mwaka huu.

Alisema mpaka sasa wameshanunua takribani tani 26,000 kutoka kwa wakulima kwa bei elekezi iliyowekwa na serikali.

"Serikali kupitia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan imetuelekeza kununua kilo moja ya mahindi kutoka kwa wakulima kwa Sh.700, na mpunga kwa Sh. 900," alisema.

**"Serikali kupitia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan imetuelekeza kununua kilo moja ya mahindi kutoka kwa wakulima kwa Sh.700, na mpunga kwa Sh. 900," alisema.**

Range alisema kumekuwa na mwamko mkubwa miongoni mwa wakulima wengi wa mazao hayo kuuza nafaka zao katika soko hilo.

Alisema: "Kutokana na wingi wa wakulima kuleta nafaka zao, tumeamua kufungua vituo 12 vya kununulia nafaka katika maeneo yote ndani ya kanda yetu ili kuwapunguzia wakulima usumbufu na gharama za kusafirisha nafaka zao umbali mrefu".

Alivitaja vituo hivyo ni Namanyere, Mtenga na Kasu vilivyopo katika Wilaya ya Nkasi, Matai, Mwimbi, Katazi na Mkobo (Wilaya ya Kalambo) Mtowisa, Laela na Kaengesa (Sumbawanga vijijini), pamoja na Kanondo, na Mazwi vilivyopo Manispaa ya Sumbawanga.

Amesema mradi huo umegharimu Dola za Marekani milioni 6.19, kuwezesha ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za nafaka, pamoja na vihenge vya kisasa vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 20,000.

Katika hatua nyingine, NFRA kupitia Kanda ya Sumbawanga mkoani Rukwa imeingia mkataba wa kuuza tani 250,000 za mahindi



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kushoto), akipokea maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Bima wa Benki ya NMB, Martin Masawe (kulia), alipotembelea banda la NMB kwenye ufunguzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Kitaifa uliofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema wakulima wa tumbaku, tani 61,000 zikiwasili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI ya Mbolea Tanzania (TFC) na Kiwanda cha Mbolea cha United Capital Fertilizer Zambia Company Limited (UCFL) zimesaini mkataba wa uagizaji wa mbolea tani 61,000 ya NPK kwa ajili ya kilimo cha tumbaku kwa msimu wa kilimo 2024/2025.

Mbolea hizo zitaingia nchini leo na kusambazwa kwa wakulima ili wafanye kilimo chenye tija, ambacho kitawainua kiuchumi.

Mkataba huo umesainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa TFC, Samwel Mshote na Mtendaji Mkuu wa UCFL, Huang Yaochi na kushuhudiwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo (Ushirika na Umwagiliaji), Dk. Suleiman Serera.

Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent; Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku, Stanley Mnozya.

Akizungumza wakati wa utiaji saini ya mkataba huo, Waziri wa Kilimo Hussein Bashe alisema mkataba huo utasaidia kuinua kilimo cha tumbaku nchini.

Alisema fursa hiyo inapaswa kutumiwa vema na wakulima wa tumbaku kwa sababu uhakika wa kuendeleza kilimo wanao kutokana na uwepo wa mbolea.

"Huu mkataba utaleta manufaa makubwa kwenye kilimo cha tumbaku hapa nchini, utakwenda kuwabadilisha wakulima wa zao hilo na kuachana na kilimo cha mazoea," alisema Bashe.

Pia aliwataka wakulima wa tumbaku kuwa mstari wa mbele kuchangamkia mbolea mara tu itakapoanza kutolewa.

Alisema makubaliano hayo yamelenga kuongeza tija na uzalishaji wa zao la tumbaku nchini kwa kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa mbolea ya uhakika kwa wakulima.

Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, Stanley Mnozya, aliishukuru serikali kutokana na kuridhia kusainiwa kwa mkataba huo ambao unakwenda kubadilisha kilimo cha tumbaku.

Alisema wakulima wa zao hilo wapo tayari kufanya kilimo chenye tija ambacho kinakwenda kuleta manufaa kwa wakulima.

# Mbunge akemea matukio ya mauaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MBUNGE wa Singida Kaskazini, Ramadhan Ighondo, amekemea vitendo vya mauaji kwa imani za kishirikina vinavyofanywa na baadhi ya watu wanaosaka utajiri, kwa kuua na kuchukua viungo vya mwili.

Alitoa kalipio hilo jana wakati akizungumza na gazeti hili ikiwa ni siku mbili tu baada ya miili ya watu watatu waliouawa katika Kijiji cha Makuro Halmashauri ya Singida Vijijini, kukutwa imezikwa nyumbani kwa mganga wa kienyeji.

Ighondo alisema vijana wafanye kazi wasijiingize kwenye makundi mabaya na kushawishiwa kuua watu pamoja na kunyofoa baadhi ya viungo vya miili kwa kudhani kufanya hivyo watapata utajiri.

Alisema: "Hakuna 'shortcut' kwenye kupata utajiri namna pekee ya kupata maisha mazuri ni kufanya kazi halali, nalaani mauaji haya ambayo yametokea jimboni kwangu, naviomba vyombo vya ulinzi na usalama vichukue hatua kali kwa wahusika".

Pia aliwaasa wananchi wa jimbo hilo hususani mabalozi wa nyumba kumi wawe wanatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi kunapotokea mauaji kwenye maeneo yao, badala ya kukaa kimya na kusababisha mambo yanakuwa makubwa.

Tukio la kukutwa miili ya watu watatu imezikwa nyumbani kwa mganga wa kienyeji imezua taharuki na hasira kwa wananchi ambao waliamua kuchoma nyumba za mganga huyo.

Kufuatia hali hiyo Jeshi la Polisi Mkoa Singida limeweka kambi kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika makazi ya mganga huo na Kijiji cha Makulo. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Amon Kakwale, akizungumza na wananchi mwishoni mwa wiki alisema eneo hilo litakuwa chini ya jeshi hilo mpaka taratibu zote zitakapokamilika.

# 'Toeni taarifa matukio ukatili wa kijinsia'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAMII imetakiwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi nchini kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia ili watuhumiwa wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Ofisa kutoka shirika lisilo la kiserikali la Msichana Inniciative, Francis Shayo alibainisha hayo juzi wakati akifungua semina ya walimu kutoka baadhi ya mikoa nchini kuhusu namna ya kupinga ukatili.

Francis alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Rebeca Gyumi.

Alisema kumekuwa na matukio mengi ya ukatili nchini lakini baadhi ya watu hawatoi taarifa kwa vyombo vya sheria ili wahusika wakamatwe na kupewa adhabu stahiki.

Aidha, alisema semina hiyo imelenga kuwajengea uwezo walimu namna bora ya kukabiliana na masuala ya ukatili wa kijinsia.

"Natunaamini walimu wanakwenda kuwa mabalozi wazuri wa masuala ya ukatili watatoa pia mafunzo kwa wengine ya kupinga ukatili katika jamii zao," alisema Shayo.

Alisema katika utekelezaji wa masuala ya kupinga ukatili wamekuwa wakikutana na changamoto mbalimbali ikiwamo hiyo ya kutoa ushirikiano wa utoaji wa taarifa.

Hata hivyo, alisema katika moja ya mikakati yao ni kuhakikisha kuwa ukatili wa kijinsia unatokomezwa ikiwamo wahalifu wa masuala hayo kukamatwa.

Aidha, alisema lengo la shirika hilo ni kuona kila mmoja anakuwa mlinzi wa mwenzake katika kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake.

Alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa walimu kwa sababu wanaamini kundi litatoa elimu shuleni, pia kutoa ushirikiano kwa madawati ya jinsia ili wahusika wanakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.





# Upungufu wa walimu wawaliza wazazi Makambako

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa vitongoji vya Nyambogo na Mtamba Halmashauri ya Makambako mkoani Njombe, wameiomba serikali kuajiri walimu ili kuwaondolea adha wazazi ya kuajiri walimu wa kujitolea.

Walitoa ombi hilo juzi katika mkutano wa kusikiliza kero za wananchi wa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka uliofanyika Kijiji cha Ukelu Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Walisema katika vitongoji vyao zipo shule mbili za msingi ambazo zinauhaba wa walimu.

"Kilio chetu kwa serikali kwamba kama ikiwapendeza tuweze kupata watumishi, maana yake imefika mahali sisi wazazi tumeanza kuajiri walimu wa kujitolea," alisema Riston Nyika.

Ezebio Mlimbila aliiomba serikali kuharakisha suala la kuajiri walimu kwa sababu wazazi wanapata adha kubwa kuajiri walimu kwa kipato chao ambacho ni kidogo.

Clement Mwagike alisema pia lipo wimbi kubwa la watoto kuhitimu kidato cha nne na kubaki mitaani bila ya kuwa na kazi yoyote na kutumia fursa hiyo kuiomba serikali kuwajengea chuo cha ufundi katika kijiji chao, ili kukabiliana na tatizo la ajira.

Naye Robert Andrew alisema wakazi wa Kitongoji cha Mjimwema wanakabiliwa na tatizo la kukosekana kwa mnara wa simu na kueleza kuwa wanapata shida kutumia simu kwa ajili ya mawasiliano.

**"Serikali inakwenda kubadilisha mitaala, hawa watoto walipo darasa la pili mwaka huu hawatasoma hadi darasa la saba, watasoma wataishia la sita na elimu ya msingi kwa Tanzania haitaishia la saba," alisema.**

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema kero zilizowasilishwa na wananchi hao zitafanyiwa kazi ili kuwaondolea adha wazazi na wanafunzi waweze kupata elimu bora. Mtaka alisema serikali imepitia mitaala yote ikabaini kwamba kuna tatizo la watoto kumaliza elimu ya msingi na sekondari wanapata shida ya ajira.

"Serikali inakwenda kubadilisha mitaala, hawa watoto walipo darasa la pili mwaka huu hawatasoma hadi darasa la saba, watasoma wataishia la sita na elimu ya msingi kwa Tanzania haitaishia la saba," alisema.

Alisema pia serikali imebadilisha mitaala kwamba wameongeza na kuboresha mitaala kwenye masomo ambayo yatamwezesha mtoto misingi ya kujitegemea kwa masomo ya ujasiriamali, stadi za maisha, ufundi, ugunduzi na uvumbuzi.



Kazi ya ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendokasi ikiendelea katika barabara ya Bagamoyo eneo la Afrikana, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima wa chai walia ubovu miundombinu, viwanda

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa chai katika Tarafa ya Lupembe Wilaya ya Njombe mkoani Njombe, wameiomba serikali kujenga viwanda na miundombinu ya barabara kuelekea maeneo yenye uwekezaji wa zao hilo.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa uzinduzi wa chai imara kutoka Kampuni ya Homsa iliyofanyika wilayani hapa juzi.

Wakulima hao akiwamo Godlove Nyalusi alisema adha iliyopo ni kwamba viwanda havifanyi kazi ipasavyo na soko la chai siyo zuri.

"Malipo yetu hayalipwi kwa wakati hali ambayo inasababisha sisi wakulima kuona kwamba zao hili hivi sasa halitufai, tunaomba sana serikali itusaidie," alisema Nyalusi.

Nyalusi alisema kutokana na kero hizo wakulima wengi wametelekeza mashamba yao kwa madai ya kupata hasara katika uwekezaji wao.

Naye Peter Kisogo alisema kuna tatizo la barabara mbovu zinazoelekea mashambani pamoja na kupanda kwa bei ya pembejeo za kilimo.

Alisema hali hiyo imechangia anguko la kilimo cha chai Lupembe, hivyo kuiomba serikali kutafuta mwarobaini wa vikwazo hivyo ili kuinua tena kilimo hicho.

"Tuombe serikali iweze kuona ni namna gani inakwenda kusaidia kuondoa kero hizo za barabara ambazo zimekuwa hazipitiki hasa kipindi cha mvua nyingi," alisema Kisogo.

Jimson Muhomisoli alisema hapo awali wawekezaji walikuwa wakinunua chai kwa wakulima halafu hawawalipi kwa wakati, hali ambayo imesababisha hata vijana kuachana na kilimo hicho. Mtaalamu wa kilimo kutoka Kampuni ya Homsa, Mathias Kaberege, alisema wameamua kuleta mapinduzi ya kilimo kwenye zao la chai na hivyo kuwataka wakulima kuondoa hofu sababu wamejipanga kununua chai ili kuleta tija. Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swalle aliwataka wakulima kumlinda mwekezaji huyo ambaye amekubali kuinua tena sekta ya chai Lupembe na kujiepusha na migogoro.

# Wazazi wakumbushwa kuongeza nguvu katika malezi

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

WAZAZI na walezi Manispaa ya Iringa mkoani Iringa, wametakiwa kuongeza nguvu katika kuwasimamia watoto wao katika malezi, ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili na mmomonyoko wa maadili.

Katika siku za hivi karibuni Mkoa wa Iringa umetajwa kukumbwa na matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwamo vitendo vya ulawiti na ubakaji, hali inayotishia usalama na ustawi watoto shuleni na nyumbani.

Akizungumza na wazazi waliohudhuria mahafali ya kwanza ya darasa la saba katika Shule ya Msingi Good Victory iliyopo Kata ya Isakalilo, Kaimu Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Iringa, Roda kinyamagoha, alikumbusha jamii juu ya wajibu wao katika malezi ili kuwa na kizazi bora kitakacholisaidia taifa.

Alisema licha ya wazazi na walezi kuwa na majukumu mengi ya kutafuta kipato ili kuendesha maisha yao lakini wanao wajibu wa kulinda na kuwahakikishia usalama watoto wao.

"Wazazi wengi tunaelewa namna dunia ilivyobadilika hasa katika ongezeko la vitendo vya ukatili, katika mkoa wetu tumesikia namna wimbi la vitendo vya ubakaji na ulawiti vilivyoshamiri, hivyo ni wajibu wa kila mzazi kumlinda mtoto wake na mtoto wa jirani ili asifanyiwe vitendo hiyo," alisema Kinyamagoha.

Diwani wa Kata ya Isamilo, Deogratus Msemwa aliwataka wazazi kutoruhusu wageni, ndugu kulala na watoto wao kwa sababu vitendo vingi vya ukatili vinaanzia ngazi za familia, kwamba hutumia mbinu za kuwatisha watoto wasitoe taarifa kwa wazazi.

Alisema: "Siku hizi mambo ya ujomba na ushemeji tuweke pembeni, wapo baadhi yetu ambao watoto wao wamefanyiwa ukatili wa kulawitiwa na kubakwa na watu wa karibu ambao waliwaamini wakawakaribisha nyumbani lakini mimi leo nasema ujomba na ushemeji tuweke pembeni akija mlaze jikoni."

Meneja wa Shule ya Good Victory, Eunice Kimati, alisema wamekuwa wakifundisha watoto kuishi kwa misingi na tamaduni za kitanzania pamoja na kutambua mabadiliko ya teknolojia.

"Tunahakikisha tunawafundisha wanafunzi wetu kuwa mabalozi wazuri katika kukemea vitendo viovu wawapo nyumbani, hivyo tunaamini pindi wanapohitimu tutakuwa na jamii yenye watu salama na wanaoweza kukemea maovu," alisema Kimati.

Kimati alisema serikali imesaidia kuboresha mazingira mazuri katika sekta ya elimu nchini na kuchochea ufanisi katika utoaji wa elimu bora kwa watoto.

Baadhi ya wazazi akiwamo, Steven Mwasaka na Sophia Mwambwiga, walisema kwa sasa wazazi wanapaswa kurudi katika misingi ya malezi, ili kuhakikisha watoto wanalindwa badala ya kujikita katika kutafuta fedha pekee.



# Ufisadi leseni uingizaji vileo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA) imesema mabadiliko yaliyofanywa kwenye utoaji wa leseni za kuingiza vileo visiwani humo hayana tija kutokana na kughubikwa na vitendo vya ufisadi.

Hayo yamo katika ripoti ya uchunguzi uliofanywa na timu ya ZRA ambayo pamoja na mambo mengine imebaini hasara kubwa za kikodi kati ya Januari na Juni mwaka huu kutokana na vitendo hivyo.

Uchunguzi huo umeendelea kubaini takriban waagizaji wote wa vileo vinavyoruhusiwa na Bodi ya Vileo Zanzibar hawana mfumo mzuri wa kuandaa taarifa zao za biashara.

"Hakuna mfumo mzuri wa udhibiti wa hisa unaoruhusu kuona mwenendo wa hisa kwa kulinganisha na hati za uingizaji na pia hakuna uzingatiaji wa utoaji wa risiti za elektroniki (VFMS)," ripoti hiyo inasema.

ZRA katika ripoti hiyo ya uchunguzi imebaini mmoja wa waagizaji wa leseni hana uwezo wa fedha kuendesha biashara ya vileo Zanzibar badala yake wanatumia faida ya kuwa na leseni ya bodi kwa kumtumia mfanyabiashara mwingine kutoka Dar es Salaam kwa niaba yao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kampuni ya mfanyabiashara hiyo, haijawahi kulipa kodi ya marejesho ya Ongezeko la Thamani (VAT) tangu ilipoanza biashara hadi Juni mwaka huu kwa sababu ununuzi wao ni mkubwa ikilinganishwa na mauzo yao madogo.

Ripoti hiyo imeendelea kubaini kuwa mchakato wa kuagiza pombe katika Bandari ya Zanzibar hauridhishi, waagizaji wengi huondoa mizigo yao nje ya bandari usiku na kuna uwezekano wa kutangazwa kwa mizigo inayotoka nje ya nchi.

"Kampuni moja wanatumia eneo la Forodhani kupeleka mizigo yao, ambapo hakuna ofisa wa ushuru anayekagua mizigo iliyotoka nje," ZRA inaendelea kueleza katika ripoti yake hiyo. ZRA imebaini baadhi ya baa na migahawa hufanya kazi kama wasambazaji wa vileo kinyume na leseni zao za biashara, na wanachouza hakitoi risiti zinazofaa kwa sababu manunuzi hayakufanywa kwa VFMS.

> **"Kampuni moja wanatumia eneo la Forodhani kupeleka mizigo yao, ambapo hakuna ofisa wa ushuru anayekagua mizigo iliyotoka nje," ZRA inaendelea kueleza katika ripoti yake hiyo.**

Aidha, kuna uwezekano mkubwa wa ukwepaji wa kodi makusudi unaofanywa na waagizaji hao wapya wenye leseni kwa sababu kodi inayolipwa na wao ni chini ya asilimia 10. Ripoti hiyo inasema kuwa baa nyingi na klabu za usiku zinanunua pombe za magendo kwa sababu hazijasajiliwa VAT kwa hivyo hazihitaji risiti ya VFMS kwa sababu haziwezi kuzitumia kama ongezeko hilo la thamani ya pembejeo.

Hakuna taarifa za kukamatwa kwa pombe za magendo kutoka Kikosi Maalumu cha Kudhibiti Magendo (KMKM) ambazo zimefika Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo mwaka huu badala yake kuna taarifa za kutorosha bidhaa nyingine za vyakula mfano mafuta ya kula, mchele na sukari.

Ripoti ya ZRA pia imegundua kuwa hakuna ugavi thabiti wa vileo kwa hoteli za kitalii kwa sababu ya kushindwa kutoa risiti za VFMS. "Hakuna udhibiti mzuri katika Bandari ya Malindi upande ambao meli kutoka Dar es Salaam zinatia nanga. Uchunguzi wetu mfupi ulionyesha ni ofisa ushuru mmoja tu ndiye anayesimamia ukaguzi mapema asubuhi meli zinapokuja," ripoti imesema.

Uchunguzi wa ZRA umebaini kuna uwezekano wa baadhi ya bia na pombe kali za viloba kutoka nje ya nchi huingizwa nchini kwa malori yanayobeba bidhaa za vyakula kutoka Dar es Salaam ambapo ni vigumu kukagua ndani ya lori hilo kwa sababu ya miundombinu ya Bandari ya Zanzibar haina nafasi ya kutosha. Inaeleza kuwa meli zinapotoka Bandari ya Dar es Salaam katika upande huu wa Bandari ya Malindi hakuna mashine ya kukagua bidhaa kutoka nje. Bodi ya Kudhibiti Vileo Zanzibar (ZLCB) ambayo ni Bodi ya Ushauri ya Udhibiti wa Vileo visiwani humo iliyoanzishwa chini ya Sheria Namba 9 ya mwaka 2020 ilifanya mabadiliko mwaka jana katika utoaji wa leseni.

Licha ya mabadiliko hayo kupingwa, mwanzoni mwa mwaka huu, bodi hiyo ilizielekeza taasisi mbalimbali ikiwamo ZRA kuhusiana na mabadiliko yaliyofanywa kwenye utoaji leseni za kuingiza vileo Zanzibar.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga (kulia), pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Zanzibar, Rahim Baloo, wakiwa katika mkokoteni wa ng'ombe katika Maonesho ya Utamaduni wa Mswahili wa Kipemba wakati wa Tamasha la Mswahili wa Kipemba lililofanyika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete-Pemba, tamasha hilo lilifunguliwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Mkuu ataja chanzo kukithiri migogoro ya ndoa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhani Abdallah, amekitaja chanzo cha kukithiri kwa migogoro ya ndoa na udhalilishaji visiwani hapa ni jamii kushindwa kutambua misingi ya dini yao.

Abdallah aliyasema hayo baada ya kukagua eneo la kufanyia ibada maalumu ya kimataifa ya Ijitmai lililoko Kidoti Mkoa wa Kaskazini Unguja mwishoni mwa Oktoba mwaka huu.

Alisema ikiwa jamii itaelimika na kutambua umuhimu wa kulea ndoa zao katika misingi bora anayoiridhia Mwenyezi Mungu, kutakuwa na jamii bora na zenye kufuata maadili mema ya dini hiyo ya kiislamu.

Aliitaka jumuiya hiyo kuikumbusha jamii umuhimu wa kutunza ndoa zao na kulea vizazi vyao kama miongozo ya dini inavyoelekeza. Alisema ikiwa taaluma hiyo itatolewa ipasavyo kesi za migogoro ya ndoa zitapungua mahakamani.

"Tunazo mahakama za kadhi hapa Zanzibar, lakini zimekuwa zikielemewa na kesi nyingi za migogoro ya ndoa ambayo imekuwa ikishamiri siku hadi siku," alisema. Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A', Othman Ali Maulid, alisema wilaya hiyo imeweka mikakati kuhakikisha Ijitmai hiyo inafanikiwa kwa kuimarisha ulinzi na usalama wakati wote wa maandalizi hadi mwisho wake.

Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Othmani Ame Chum, aliahidi wataendelea kuunga mkono juhudi za jumuiya hiyo ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Vilevile Chum, alisema ataendelea kuielimisha jamii umuhimu wa kutenda mema na kukataza mabaya.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza katika harakati hizo, walisema nguvu kazi inahitaji kukamilisha ujenzi na kuweka hali ya usafi katika eneo hilo.

Mwajuma Said, alisema mazingira yakiwa safi na salama yatawafanya waislamu watakaofika eneo hilo kufanya ibada zao.

# Wizara yatakiwa kuboresha vivutio vya utalii Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imetakiwa kuboresha vivutio vya utalii vilivyoko Kisiwa cha Pemba ili kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa.

Rai hiyo imetolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla katika Tamasha la Mswahili wa Kipemba lililofanyika ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi Wete Pemba.

Abdulla, alisema serikali imeweka adhma ya kuifungua Pemba kiuchumi kupitia sekta ya utalii kwa wageni na wakazi wa kisiwa hicho.

Alisema serikali imelipa kipaumbele suala la utalii ili kukuza uchumi wa Zanzibar, hivyo ni lazima kuimarisha mila, silka na utamaduni wa watu wao kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Alisema katika kufika malengo iliyojiwekea ya kuifungua Pemba kiuchumi, serikali inaendelea kuchukua hatua kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kujenga barabara kuu na za ndani ili kurahisisha usafiri wa wananchi, wageni, bidhaa na kukuza uchumi.

Alisema serikali pia inakamilisha utaratibu wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba wenye hadhi ya kimataifa kwa ajili ya kuleta watalii moja kwa moja kutoka nchi zao hadi Pemba.

Sambamba na Abulla aliigiza wizara hiyo kuhakikisha wageni wanaoingia katika Unguja wanapata fursa ya kufika Pemba kuongeza jitihada za kutangaza vivutio vya utalii kitaifa, kimataifa vilivyoko katika visiwa hivyo.

Waziri wa wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema tamasha hilo la Mswahili wa Kipemba linafanyika kwa lengo la kuifungua Pemba kupitia uwekezaji na utalii ili wananchi waweze kutambua fursa zinazopatikana katika sekta hizo.

Soraga, alisema Pemba ni eneo la kimkakati katika Sekta ya Utalii, hivyo kila mmoja awe balozi wa kutangaza fursa zilizopo kisiwani humo kitaifa na kimataifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Zanzibar, Rahim Baloo, alisema azma ya serikali ni kuona utalii unakua na kuimarika zaidi kwa kudumisha mila, silka na tamaduni za kipemba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

BENARD MATHIAS RWEYEMAMU anatangaza kupotea kwa Hati ya kiwanja No. **LAT. 064 KITALU No. 27 HD MAJENGO BLOCK Q .** Hati hii ya kiwanja iliungua ndani ya Nyumba. Taarifa imetolewa Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/-DOD/DOD/30205/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**No. 17525/2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**ANDERSON MAZENGO NYONG'OLE of AZIMIO CHAMWINO**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DANY MAZENGO MAZENGO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 8, 2024
Date at Dodoma this 11 Day of JULY, 2024.

Presented for filing this 22 day of 7, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FRANCIS ROBERT NYAMBIRO** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE299564** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji **DAR ES SALAAM** tarehe **13/02/2020**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/130242/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**JUMANNE KIBELA KISHIMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya guta yenye namba za usajili **MC916CRH** aina ya KINGLION, Chassis **No. KINGLION200500029.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/-**DOD/30018/2024**.

## KUPOTEA KWA CHETI



**KESHENI FRANK ULENDO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1246/0008** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MIDLANDS HIGH SCHOOL mwaka 2017**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/MBU/RB/828122/2020**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**No. 12980/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**MARIUS MATHIAS NYENZA of Ipagala Area**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAGRETH JOHN MABULA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 8, 2024
Date at Dodoma this 22 Day of 7, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**No. 17526/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**SOSPETER WAMBURA MTEI of Nkungu**
**Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARGARET DAVID NATAI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 8, 2024
Date at Dodoma this 10 Day of JULY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI SUB- REGISTRY**
**AT MOSHI**
**APPLICATION NO.9089 OF 2024**
**(REF20240425100009089)**
**MARIA RAPHAEL MUSHI AND 8 OTHERS……**
**..............................................APPLICANTS**
**VERSUS**
**THADEI PAUL MUSHI………RESPONDENT**
**TO: THADEI PAUL MUSHI.**
**NOTICE FOR HEARING,**
**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for hearing in the High Court of Tanzania at Moshi on 9th September ,2024 at 09:00 a.m. before Honourable S.P.MWAISEJE-DR.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the **NIPASHE.**
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **18th day of July ,2024.**

DEPUTY REGISTRAR
MOSHI

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MARY PETER LUKINDO** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili **T 818 BVB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/TAN/7863/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KILOLO**
**Kituo cha MAZOMBE Mkoa IRINGA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na....18.../2024....**
**Jina la mdai ...NURU JENGO.....**
**Jina la Mdaiwa ....RUKIA ATHUMANI..**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
[Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama ya Mwanzo]
Kwa..........RUKIA athumani...........
kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake /yao kwamba[Elez hapa habari za Madai]
Kwa kuwa na mgogogro wa ndoa kwa muda mrefu unaopelekea kushindwa kupata suluhu baina ya pande ya mdai na mdaiwa hivyo anaomba Mahakama itoe Talaka ,mgawanyo wa mali na matunzo ya watoto.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 17 mwezi 09 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo
Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwajili ya kujitetea
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juuna ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 08 mwaka 2024.



**DEED POLL**
**MADE UNDER THE REGISTRATION OF DOCUMENTS**
**ACT (CAP 117) R.E 2002**
BY **PENDO EDWARD LAIZER** of Arusha,Tanzania **DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use my former names **HAWA SAID MWANGU** and lieu thereof do assume names **PENDO EDWARD LAIZER.**
**AND** in pursuance of such change of my names as aforesaid,
**I HEREBY DECLARE** that I shall all times hereafter and all in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon occasions whatever use the said assumed name in lieu of the said former names of **HAWA SAID MWANGU.**
AND I HEREBY authorize and request all persons to designate address me such assumed names of **PENDO EDWARD LAIZER.**
THAT I have decided to renounce my names HAWA SAID MWANGU after being joined to my patrilineal family since I have been raised by uncle who changed my original Christianity religion of into Muslim.
**IN WITNESS THEREOF,** I have hereunto subscribed my names of **PENDO EDWARD LAIZER** and renounce the names of HAWA SAID MWANGU the day and year hereinafter written.
THAT, I have to assume my baptismal name **PENDO EDWARD LAIZER.**
SIGNED and **DELIVERD** by the said **PENDO EDWARD LAIZER**
(who was formerly known as **HAWA SAID MWANGU**
}.............
**DEPONENT**
Who is known to me personally
This 22nd day of February 2023
BEFORE ME:
Name: GONZAGA GASTO MWOMBEKI
Signature……………………………
**Address: ARUSHA**
**Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS**

**FOMU MADAI - 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA**
**Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Ndoa Na. 30/2024**
Jina la mdai: **SALUME MARCO MBALI**
Jina la mdaiwa: **ISANZU NDATULU MANG'OMBE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)
Kwa: ISANZU NDATULU MANG'OMBE WA MWATUMBE
K.K AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA MWATUMBE
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
**ANADAI TALAKA, GHARAMA ZA MATUNZO YA WATOTO SH. 100,000/- NA CHUMO LA PAMOJA**
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 mwezi wa 08 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 Mwezi 08 Mwaka 2024

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEIF RAJABU YUSUF** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 193 AAR – TOYOTA LANDCRUISER PRADO.** Chassis namba KZJ780020567. Engine namba **1K20071776.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/177014/2024.**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

Ndugu **STEPHEN PHARES DAUD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye namba za usajiri **T. 592 DDY** na Chassis Namba **ANH100147157.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/8768/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**YESE ANANIA SINKAMBA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE352400** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji **DAR ES SALAAM** tarehe **06/08/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SON/MOM/6279/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na…34/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SELEMANI ABDUL SELEMANI. WA MOROGORO.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAMADHANI SELEMANI ABDUL.**
**ZUHURA MOHAMED MKIYA.**
**TANGAZO**
***(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 09 Mwezi 09 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 8 mwaka 2024**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Chanjo ya Mpox kuwasili Afrika wiki hii

**AFRIKA**

DOZI 10,000 za chanjo ya Mpox ambazo ni za kwanza zinatarajiwa kuwasili barani Afrika kuanzia wiki hii, wakati huu pia maambukizo zaidi yakiendelea kuripotiwa hali iliyofanya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza ugonjwa huo kama janga la kidunia.

Ilielezwa kuwa chanjo hizo zinaletwa Afrika baada ya mataifa zaidi ya 70 nje ya bara hilo kuwa nazo, likiwa ni dhihirisho kuwa mafunzo kutokana na Uviko-19 ambako Afrika ilibaguliwa katika usambazaji wa chanjo, bado hayajaweza kuleta mabadiliko.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Kudhibiti Magonjwa Barani Afrika (CDC), ucheleweshaji huo ambao umelazimu Afrika kutegemea chanjo za msaada ni kuwasababu kampuni za kuzalisha chanjo zilihitaji kupata idhini kutoka WHO, ruhusa ambayo imetolewa mwezi huu.

Ilielezwa kuwa gharama ya kununua chanjo moja kwa moja imekuwa changamoto ambayo inalazimu Afrika kutegemea ununuzi unaofanywa kupitia muungano wa GAVI mpango ambao pia unahitaji muda.

Pia ilibainishwa kuwa hadi kufikia sasa kuna aina mbili za chanjo, moja inayotengenezwa na kampuni ya Denmark ya Bavarian Nordic inayogharimu dola mia moja kwa dozi, na ile inayozalishwa na kampuni ya Japan KM Biologics ambayo bei yake bado haifahamiki.

Kwa mujibu wa CDC, Afrika ina uhitaji wa dozi milioni kumi, na imekuwa na dozi laki mbili, ambazo zimeelekezwa zaidi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambayo imeathirika zaidi na Mpox.

Katika hatua nyingine, Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis alitoa wito kwa serikali na kampuni za kutengeneza dawa duniani kufanya kazi ya ziada ili kupeleka chanjo dhidi ya ugonjwa huo kwa mataifa yaliyoathirika.

Papa Francis alisema anawaombea watu wote walioambukizwa wapate nafuu ya haraka, hasa raia wa DRC waliokutwa na Mpox, huku WHO ikihimiza kutengenezwa na kusambazwa zaidi chanjo ya ugonjwa huo.

Mpox imeenea zaidi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 570 mwaka huu. Na kwamba mataifa mengine yaliyokumbwa na ugonjwa huo ni Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda na mgonjwa wa kwanza wa mpox aliripotiwa nchini Sweden wiki iliyopita.

**RFI, DW**

## Ukraine yaisisitiza Belarus kuondoa wanajeshi mpakani

**KYIV,** Ukraine

UKRAINE imeisisitiza Belarus kuondoa kile walichokieleza kuwa ni idadi kubwa ya vikosi vya kijeshi vya nchi hiyo na zana za kivita kwenye mpaka wao wa pamoja.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje ya Ukraine, ambayo iliionya Belarus dhidi ya kufanya makosa ya kusikitisha wakati ikishinikizwa na Russia.

Wizara hiyo ilivihimiza vikosi vya Jeshi la Belarus kuacha vitendo visivyo vya kirafiki na kuondoa wanajeshi wake mpakani.

"Vikosi maalum vya jeshi la Belarus pamoja na wapiganaji wa zamani wa kundi la mamluki la Russia Wagner walikuwa miongoni mwa wanajeshi walioko mpakani," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Ilielezwa kuwa miongoni mwa zana za vita za Belarus ni pamoja na vifaru, makombora, mifumo ya ulinzi wa anga na vifaa vya uhandisi vilivyopelekwa katika mkoa wa Gomel karibu na mpaka wa Ukraine upande wa kaskazini.

Wizara hiyo ilisema Ukraine haijawahi kuchukua na haina nia ya kuchukua hatua yoyote isiyo ya kirafiki dhidi ya watu wa Belarus.

Pia ilielezwa kuwa Agosti 18, mwaka huu, Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko, alisema kuwa Ukraine ilipeleka zaidi ya wanajeshi 120,000 kwenye mpaka wa nchi hizo mbili.

Mamlaka nchini humo ilisema jana kuwa imetuma ndege, vikosi vya ulinzi wa anga na vifaru vya kivita kwenye mpaka wake na Ukraine.

Belarus ambayo inashirikiana na Russia, haijihusishi moja kwa moja na vita kati ya Russia na Ukraine.

Hata hivyo, Lukashenko aliruhusu wanajeshi wa Russia kuingia Ukraine kupitia Belarus wakati wa uvamizi wake uliotekelezwa Februari 2022.

Vile vile, ilielezwa kuwa baada ya kushindwa na kupata hasara kubwa wakati wa jaribio la kusonga mbele na kuelekea mjini Kyiv, vikosi vya Russia hatimaye vililazimika kujiondoa. **DW**



Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, akiwaombea watoto alipofanya ziara katika kambi ya wakimbizi mjini Bangui, DRC. **PICHA: MTANDAO**

## Kenya yatuma wanajeshi kulinda amani DRC

**NAIROBI,** Kenya

KENYA imetuma wanajeshi wake nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kujiunga na kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa (UN) chenye jukumu la kurejesha utulivu katika eneo lenye machafuko mashariki mwa nchi hiyo.

Hayo yalibainishwa jana kupitia taarifa iliyotolewa na Jeshi la Ulinzi la Kenya, ambalo lilisema kundi la kwanza la msaada wa haraka (KENQRF 4) lilitumwa rasmi DRC Agosti 24, mwaka huu kuashiria kuanza kwa misheni yao ya kulinda amani nchini humo.

Lilisema kikosi hicho kitashiriki katika operesheni dhidi ya vikundi vyenye silaha, kulinda raia, kusaidia juhudi za kibinadamu, kuwapokonya silaha, kuwaangamiza, na kuwajumuisha tena wapiganaji wa zamani.

"Kikosi hicho kitaungana na Kikosi cha Kulinda Utulivu cha Umoja wa Mataifa huko DRC, (MONUSCO), ambacho kinalenga kuleta utulivu katika maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo, ambako makundi yenye silaha yanaendelea kusababisha uharibifu." Ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Luteni Kanali Simon Seda, kamanda wa KENQRF 4, alionyesha imani kwamba wanajeshi walikuwa wamejitayarisha vyema kwa misheni hiyo wangeleta athari chanya katika kutumwa kwao.

"Wanaume na wanawake wetu wamejiandaa kwa kazi iliyo mbele yao. Wamepitia mafunzo makali na wamepewa ujuzi unaohitajika ili kutekeleza misheni hii kwa ufanisi. Tumejitolea kuchangia katika kurejesha amani na utulivu nchini DRC," alisema.

Kwa takriban miongo mitatu, mashariki mwa DRC yamekuwa yakikabiliwa na ukosefu wa usalama unaoletwa na makundi kadhaa yenye silaha, huku maelfu ya watu wakiishi katika kambi kwenye majimbo mawili yaliyoathiriwa zaidi na migogoro ambayo ni Kivu Kaskazini na Ituri.

Ilielezwa kuwa takriban watu milioni 6.9 wanakadiriwa kukimbia makazi yao kutokana na migogoro tangu Machi 2022.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa katikati ya mapigano hayo, nchi kadhaa za Afrika sasa zina wanajeshi nchini DRC zikiwamo Tanzania, Burundi, Uganda, Afrika Kusini na Malawi. **TRT**

# SIMBA QUEENS YATOLEWA LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

SAFARI ya timu ya soka wanawake, Simba Queens, kuelekea kwenye fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika, imetamatika baada ya kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Police Bullets ya Kenya, katika mchezo mgumu wa nusu fainali Kanda ya Afrika Mashariki na Kati (CACAFA), uliochezwa Uwanja wa Abebe Bikila nchini Ethiopia jana.

Dalili za Simba Queens kushindwa kufikia rekodi yao ya 2022, ilipofika hatua ya nusu fainali kwenye hatua za fainali ya Ligi ya Mabingwa zilizofanyika nchini Morocco, zilianza kuonekana dakika za mwanzo tu iliporuhusu bao lililofungwa na Annedy Kudu, lakini baadaye lilisawazishwa na Vivian Corazone, na mechi hiyo ikaenda mapumziko kwa sare ya bao 1-1.

Vivian aliipatia Simba Queens bao la pili, lakini baada ya hapo Wakenya walionekana kucharuka na kusawazisha bao lililowekwa wavuni na Rebecca Akinyi, kabla ya Diana Wacera kupachika la tatu kwa kichwa kutokana na mpira wa adhabu ndogo, ambapo mabeki wa timu hiyo walishindwa kuruka naye.

Kwa ushindi huo, Police Bullets, imetinga hatua ya fainali, ikisubiri mshindi kati ya CBE ya Ethiopia dhidi ya Kawempe Muslim Ladies ya Uganda, mchezo ambao ulitarajiwa kuchezwa jana kwenye uwanja huo.

Hii ni mara ya pili kwa Simba Queens kushindwa kufuzu fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA, kwani iliwahi kufanyiwa hivyo mwaka 2021, ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Vihiga Queens katika mchezo wa nusu fainali uliopigwa Uwanja wa Nyayo nchini Uganda, ingawa mwaka uliofuata walitwaa ubingwa wa CECAFA nchini kwa kuitandika She Corporates ya Uganda bao 1-0 katika mchezo wa fainali Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na kupata tiketi ya kucheza fainali zake nchini Morocco.

## UNAPITAJE HAPA!...



Mchezaji wa Timu ya Soka ya Bulls chini ya miaka 16, Said Mbinga (kulia), akimzuia mchezaji wa timu ya Magnet, katika mchezo wa kirafiki uliochezwa viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mudathir afichua siri mechi Vital'O

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Mudathir Yahaya, amefichua kuwa lengo lao katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya awali dhidi ya Vital'O ya Burundi, uliochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, walipanga kushinda mabao 8-0, lakini kwa bahati mbaya ilishindikana yakaishia 6-0.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mudathir ambaye alikuwa mmoja wa waliofunga idadi katika mabao hayo, alisema yeye mwenyewe alikuwa anataka kufunga mawili, lakini pia ilishindikana.

Mudathir, alisema wachezaji wote pamoja na kocha wao, Miguel Gamondi walikuwa na idadi yao ya mabao ambayo wamejiwekea kushinda katika mchezo huo.

Alisema kwa sababu hiyo ndiyo maana alikuwa anawahimiza wachezaji wenzake kwenda kuweka mpira kati kila bao lilipokuwa limepatikana.

"Lengo letu katika mechi ile ni mabao 8-0, ndiyo maana wakati nipo benchi nilikuwa nawahimiza wachezaji waliokuwa ndani kwenda kuweka mpira haraka, kwa sababu wote sisi wachezaji na kocha tulitaka kushinda idadi hiyo ya mabao.

"Wakati naingia kocha naye akaniambia nataka uende kufunga mabao mawili, lakini sikufanikiwa nimefunga moja, nafasi zimetengenezwa nyingi baadhi hatukuzitumia, ila lengo letu kubwa ilikuwa ni kushinda mabao 8-0," alisema Mudathir.

Waliofunga mabao katika mchezo huo ni Pacome Zouzoua kwa penalti dakika ya 14, Clement Mzize dakika ya 49, Clatous Chama dakika ya 51, Prince Dube dakika ya 71, Stephane Aziz Ki dakika ya 78 na Mudathir dakika ya 86.

Chama, alitoa ‚asisti' nne katika mchezo huo, ambao uliifanya Yanga kutinga raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 10-0, baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa uwanjani hapo, Agosti 17, mwaka huu, na kushinda 4-0.

Mabao katika mchezo wa kwanza yalifungwa na Dube dakika ya sita, Chama dakika ya 68, Mzize dakika ya 74 na Aziz Ki kwa penalti dakika ya 90.

Kiungo huyo, amesema jeuri ya kupanga hata idadi ya mabao inatokana na kuwa, mbali na uwezo wa mwalimu wao, lakini wana viungo ambao wana uwezo wa kutoa pasi za mwisho za mabao, lakini pia kufunga, wakichangiwa na mastraika ambao wana uchu wa mabao.

"Msimu huu tuna viungo wenye uwezo mkubwa wa kutengeneza nafasi, lakini pia kuna wachezaji ambao wanaweza kuzitumia nafasi zinazopatikana ndiyo maana tunakuwa na uhakika wa kufunga mabao katika mchezo wowote, inategemea na mpinzani mwenyewe uzito wake, halafu pia sisi wote tunafunga.

"Viungo wetu ni wafungaji wazuri nikiwamo mimi mwenyewe na msimu huu tumepata mastraika wafungaji. kwa hiyo, wanachama na mashabiki wa Yanga ni kicheko tu," alitamba mchezaji huyo ambaye amekuwa na mwendelezo mzuri wa kufunga mabao katika mechi mbalimbali za kimataifa na Ligi Kuu Bara.

## Judo kupigwa Novemba Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya klabu ya mchezo wa Judo Afrika Mashariki yanatarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, jijini Dar es Salaam, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Judo Tanzania (JATA), Inocent Malya, alisema kamati ya utendaji itakutana wiki hii ili kupanga tarehe rasmi ya mashindano.

„Tanzania itakuwa mwenyeji wa mashindano hayo, hivyo kamati itakutana wiki hii na kupanga tarehe ambayo yatafanyika mashindano hayo," alisema Malya.

Hata hivyo, alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vizuri kwani kila mchezaji anafanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha viwango vyao.

Katibu huyo alisema baada ya kamati hiyo kukutana watatoa taarifa ili Watanzania pamoja na wadau wao wafahamu kile kinachoendelea.

## Stand Utd yasajili nyota wapya 14

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumchukua kocha mzoefu, Meja mstaafu, Abdul Mingange, Klabu ya Stand United, imefanya usajili wa wachezaji wapya 14, ambao wanatarajia kuichezea timu hiyo kwenye Ligi ya Championship ili kuirejesha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo yenye maskani yake mkoani Shinyanga, imesema inaamini mchanganyiko wa wachezaji iliyowasajili wanaweza kuirejesha timu hiyo Ligi Kuu, baada ya kuteremka msimu wa 2018/19.

Klabu hiyo imetangaza wachezaji iliyowasajili kwa ajili ya ligi hiyo inayotarajiwa kuanza mwezi ujao ni magolikipa, John Mwanda kutoka Pamba Jiji na Ismail Salehe (JKT Tanzania), Ally Hamisi, Mudrick Salim, Frank Sekule (Biashara United), Boniphace Shaaban, Emmanuel Manyanda na Ludovick Charles.

Wengine ni Emmanuel Mwita, Nassor Idd, Paschal Mahona, Abbas Athumani, Hosea Shemson na Hashim Said.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUMBADILI STERLING

CHELSEA ina nia ya kumnunua winga wa Manchester United, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 24, na huenda wakamjumuisha Raheem Sterling (29), katika mkataba wa kubadilishana wachezaji. (***Telegraph***)

### OSIMHEN AKOMALIWA

CHELSEA imeanza tena mazungumzo na Klabu ya Napoli kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, huku masharti yakiwa mazuri zaidi kwa klabu hiyo ya England. (***Sky Sports***)

### UGARTE ATAFUTIWA NJIA

KUMUUZA kiungo wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27, kwa Napoli kutaimarisha harakati za Manchester United kumnunua kiungo wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye miaka 23, ambaye klabu yake ya Paris St-Germain inataka kumuuza kwa pauni milioni 51. (ESPN)

### NKETIAH ATAKIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25, baada ya uwezekano wake wa kwenda Nottingham Forest kutibuka. (Athletic)

### SOLER NA WEST HAM

WEST Ham inataka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Carlos Soler mwenye umri wa miaka 27 kutoka Paris St-Germain, lakini lazima wauze wachezaji kabla ya kumnunua. (***Guardian***)

### BARCO KWA MKOPO SEVILLA

MLINZI wa Brighton, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 20, anatazamiwa kujiunga na Sevilla kwa mkopo, lakini mkataba wa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina haujumuishi chaguo la kumnunua. (***Fabrizio Romano***)

### NAPOLI YAMULIKA ENGLAND

MKURUGENZI wa Napoli, Giovanni Manna, amerejea England kuendelea na mazungumzo ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Brighton na Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 23, mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku (31), na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay, 27. (***Gianluca di Marzio***)

### JEBBISON AKUBALIWA MKOPO

KLABU ya Watford imekubali mkataba wa mkopo wa msimu mzima na Bournemouth kwa ajili ya mshambuliaji, Daniel Jebbison mwenye umri wa miaka 21, mzaliwa wa Canada. (***Sky Sports***)

### WORRALL HUYOOO FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imekubali ombi la kumnunua mlinzi wa England, Joe Worrall mwenye umri wa miaka 27 kutoka Burnley. (***Football Insider***)

### CHIESA SAFI BARCA

BARCELONA wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Italia, Federico Chiesa, 26. (***ESPN***)




## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MABAO KWA MBAPPE YATAKUJA - ANCELOTTI

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema hana wasiwasi na upachikaji wa mabao wa Kylian Mbappe baada ya fowadi huyo kushindwa kuzifumania nyavu katika mechi ya pili mfululizo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Mbappe alijiunga na Madrid kwa mkataba wa miaka mitano msimu huu wa majira ya joto, na alifungua akaunti yake kwa klabu katika ushindi wao wa UEFA Super Cup dhidi ya Atalanta mapema mwezi huu.

**Hata hivyo, ushindi wa mabao 3-0 wa mabingwa hao wa LaLiga katika Uwanja wa Bernabeu dhidi ya Real Valladolid Jumapili ulimfanya Mbappe kubadilishwa baada ya dakika 86, ikiwa ni mechi yake ya pili ya ligi bila kufunga bao.**

„Inanifurahisha sana. Nimeanza Bernabeu nikishinda mchezo na tukapata pointi tatu," alisema Mbappe akiiambia Real Madrid TV baada ya mchezo.

„Ulikuwa usiku mzuri sana. Mashabiki walikuwa juu. Tulitaka kushinda mchezo wa kwanza hapa. Ni ndoto kucheza katika uwanja huu, lakini tuna mchezo mwingine Alhamisi na tunataka kushinda tena."

Kiungo Federico Valverde aliiweka Madrid mbele baada ya muda wa mapumziko, na mchezaji wa akiba Brahim Diaz aliongeza bao la pili, kabla ya mbadala wa Mbappe Endrick kufunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo dakika ya 96.

> ●●● Sidhani kama anatakiwa kucheza upande wa kushoto au kulia, atafunga tu mabao...

Akizungumza katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, Ancelotti alikanusha kuwa nafasi ya Mbappe katika mshambuliaji wa kati - badala ya kuanza pembeni - ilikuwa inapunguza uwezo wake wa kuchangia timu.

„Hapana, sifikiri hivyo hata kidogo," alisema Ancelotti. „Mbappe ni mshambuliaji wa kustaajabisha, ana kasi sana, anasonga vizuri bila mpira.

„Alikuwa na nafasi tatu. Nadhani katika nafasi hiyo atafunga, kwani huwa anafunga. Sidhani kama anatakiwa kucheza upande wa kushoto au kulia. Atafunga mabao."

Ancelotti pia alimsifu Endrick, ambaye alisajiliwa na Madrid msimu huu wa majira ya joto baada ya kufikisha miaka 18.

„Anaonekana mzuri," alisema Ancelotti. „Ana uwezo mkubwa, na kwa bao alionesha sifa zake zote. Ana udhibiti mzuri, na shuti nzuri."

Ushindi wa Madrid dhidi ya Valladolid ulikuja baada ya sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Real Mallorca wikiendi ya ufunguzi wa msimu wa LaLiga, huku wakipania kutetea ubingwa wao.

Timu hiyo kwa sasa haina viungo Jude Bellingham na Eduardo Camavinga, wote ni majeruhi, huku beki Ferland Mendy akifungiwa kucheza dhidi ya Valladolid.

Madrid itasafiri hadi Las Palmas Alhamisi, kabla ya kuwakaribisha Real Betis wikendi ijayo.




# MADUEKE AMWAGA SIFA KWA COLE PALMER

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Noni Madueke, alimmiminia sifa Cole Palmer, kutokana na ushindi wao wa mabao 6-2 dhidi ya Wolves Jumapili kwenye Ligi Kuu England.

Madueke alifunga hat-trick kipindi cha pili, huku Palmer akitoa pasi za mwisho kwa mabao yake yote matatu pale kwenye Uwanja wa Molineux wakati Chelsea ikianza msimu wao vizuri.

"Yeye ni baridi na mimi ni moto, kwa hivyo inachangnyika vizuri. Siku zote amekuwa na uwezo wa kucheza pasi sahihi kwa wakati ufaao, hivyo ni kipaji," alisema Madueke akiiambia BBC Sport.

"Leo ina maana kubwa kwa kweli, kuwa wajanja na kungoja wakati mwafaka. Mfumo unaturuhusu kuchunguza na kuweka umiliki juu uwanjani.

"Labda kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu, lakini tulipata udhibiti katika kipindi cha pili. Kwanza bao lilikuwa la bahati, la pili lilikuwa Cole Palmer, pasi mbili za uzani nililazimika kupiga hatua.

"Nimetengenezewa hat-trick, lakini zaidi ni kwamba tulishinda mchezo."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, pia alikuwa akimpongeza kocha mpya Enzo Maresca.

"Nadhani ni dhahiri kila mtu aliona alichokifanya Leicester mwaka jana, ana hasira kuhusu mtazamo wake, kuhusu maelezo madogo.

"Nadhani unaona kwamba, hata katika mchezo wa kwanza dhidi ya City, kulikuwa na mifumo mizuri ya uchezaji labda hatukuweza kumaliza, lakini leo tulikuwa kliniki.

Palmer pia alifunga bao lake la pekee na kuifanya Chelsea kuwa mbele kwa mabao 2-1 kabla ya kipindi cha mapumziko, na kabla ya Wolves kusawazisha dakika chache baadaye.

Mchezaji mpya wa Chelsea Joao Felix pia alifunga bao katika ushindi dhidi ya Wolves na kuanza kipindi chake cha pili katika klabu hiyo.

Felix alijiunga na Chelsea kwa mkataba wa miaka saba kutoka Atletico Madrid baada ya kukaa kwa mkopo kwa miezi sita na klabu hiyo ya London msimu uliopita.

# Slot aelezea hasira ya Alexander-Arnold

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Arne Slot, amesisitiza kuwa alikuwa akijaribu ,kumtunza' Trent Alexander-Arnold kwa kumbadilisha wakati wa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Brentford Jumapili katika mchezo wa Ligi Kuu England.

'Wekundu' hao walipata ushindi katika mchezo wa kwanza wa ushindani wa Slot nyumbani tangu kumrithi Jurgen Klopp kwenye dimba la Anfield. Mabao katika nusu ya pili ya Luis Diaz na Mohamed Salah yaliifanya Liverpool kuambulia pointi zote tatu.

Alexander-Arnold alitolewa dakika ya 72 na nafasi yake kuchukuliwa na Conor Bradley, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alipokuwa akielekea kwenye benchi, alionesha sura ya hasira na ilibidi azungumze na Slot mara tu aliporejea kwenye kiti chake.



Katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, Slot aliulizwa kuhusu kumwondoa Alexander-Arnold na kwa nini alikasirishwa na uamuzi wa bosi wake.

"Yeye hakuonekana kuwa na furaha baada ya kuondolewa, unamaanisha? Ninaelewa," alisema Slot.

"Kila mchezaji anataka kucheza dakika 90, lakini sidhani kama wachezaji waliokuwa kwenye benchi tangu mwanzo walifurahishwa na maamuzi niliyofanya.

"Lakini Trent alirudi kutoka timu ya taifa ambapo mwanzoni mwa mashindano alicheza sana, basi hakufanya hivyo, alikuwa na mapumziko ya wiki chache akarudi, ni mchezo wake wa tatu tu na tunapaswa kumtunza. Vilevile, kwa sababu tunamhitaji kwa msimu mzima na si mechi mbili za mwanzo pekee.

"Jambo zuri kwangu ni kwamba ana usaidizi mzuri sana na wa Conor, hivyo hiyo inamaanisha tunamtunza Trent. Lakini alicheza mchezo mzuri, ndivyo nilivyoona."

Alexander-Arnold amebakiza mwaka mmoja tu kukamilisha mkataba wake na Liverpool na amekuwa akihusishwa na uhamisho wa bure kwenda Real Madrid msimu ujao wa majira ya joto.

## Kompany asifu kiwango, Bayern ikishinda Bundesliga

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Mkuu mpya wa Bayern Munich, Vincent Kompany, alisifu mtazamo wa timu yake baada ya kutoka nyuma na kuifunga VfL Wolfsburg katika mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Jumapili.

Bao la dakika ya 82 lililofungwa na Serge Gnabry, liliwahakikishia mabingwa hao wa Ujerumani ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Wolfsburg na kumpa Kompany pointi tatu, ambaye alichukua nafasi ya Thomas Tuchel baada ya kumaliza vibaya katika nafasi ya tatu msimu uliopita, mwanzo wa ushindi katika Bundesliga.

Bayern walipata bao la kuongoza kupitia Jamal Musiala dakika ya 19, lakini walianza kipindi cha pili kwa mshangao mkubwa huku wakitoa mkwaju wa penalti sekunde chache baada ya mchezo kuanza na kufanya makosa ya ulinzi ambayo yaliwaweka wenyeji mbele.

Hata hivyo, Gnabry na Harry Kane waliungana na kunyakua bao la dakika za mwisho na kuziba pointi zote tatu kwa Bayern.


"Nilifurahia, ulikuwa mchezo wangu wa kwanza wa Bundesliga kama kocha," alisema Kompany, kocha wa zamani wa Burnley, alisema baada ya mechi.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kikubwa, kama inavyopaswa kuwa. Hatukuruhusu nafasi yoyote. Kipindi cha pili hakikuwa kizuri mwanzoni, tuliruhusu mabao mawili ya haraka. Jambo la tatu ni kwamba mtazamo wetu ulikuwa sawa mwishoni, na ndio maana tulishinda mchezo.

"Makosa yanatokea, jambo muhimu ni jinsi timu inavyofanya. Hilo lilichukua muda katika kipindi cha pili. Thomas Muller na Kingsley Coman waliingia wakiwa na mtazamo sahihi.

"Mwishoni mwa kipindi cha pili, tulikuwa na ujasiri mkubwa kushinda mchezo. Haikuwa kamili, lakini tutaendelea."

Joshua Kimmich alisema majibu ya Bayern yalikuwa mazuri katika kipindi cha pili.



## HABARI MICHEZO

### Job arejeshwa Stars, Samatta, Msuva waachwa

INATOKA UK. 24

timu atamuita kwenye kikosi wakati mwingine.

Hata hivyo, alisema kikosi ambacho amekitangaza hapo jana kina wachezaji wenye viwango vya juu na kudai anaamini kitafanya vizuri katika michezo hiyo.

Aidha, aliweka wazi kuwa lengo lake ni kufanya vizuri kwenye michezo hiyo ili waweze kufuzu na kwamba siku walizonazo kabla ya mechi hizo zinawatosha kufanya maandalizi.

Wachezaji walioitwa kuunda kikosi hicho ambacho kitaingia kambini kesho Agosti 28, ni Ally Salim, Mohamed Hussen „Tshabalala', na Edwin Balua kutoka Simba, Aboutwalib Mshery, Job, Bacca, Nickson Kibabage, Bakari Mwamnyeto, Mudathir Yahaya na Clement Mzize (Yanga), Lusajo Mwaikenda, Nathaniel Chilambo, Paschal Msindo, Adolf Mtasingwa, na Feisal Salum (Azam FC).

Wengine ni Yona Amos kutoka Pamba Jiji, Abdulmalick Zacharia (Mashujaa FC), Himid Mao (Talaal el Geish ya Misri), Novatus Dismas (Goztepe ya Uturuki), Waziri Junior (Dodoma Jiji), Cyprian Kachwele (Vancouver Whitechaps ya Canada) na Abel Josiah wa TDS TFF Academy.

Stars ipo Kundi H, kwenye michuano hiyo, pamoja na timu za Ethiopia, Guinea na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Fainali za AFCON zinatarajiwa kufanyika mwakani nchini Morocco, ambapo baada ya hapo, Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa mwenyeji kwenye fainali zitakazofuata 2027, ambapo maandalizi yake yameshaanza nchini.

# MAKAMBO AREJEA NA MABAO YAKE LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Heritier Makambo, juzi alifungua akaunti yake ya mabao katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara akichezea timu yake mpya ya Tabora United na kuiongoza kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Namungo FC.

Makambo, ambaye aliichezea Yanga msimu wa 2018/19, kabla ya kutimkia Horoya na baadaye kurejea tena Jangwani kwenye dirisha dogo la msimu wa 2022/23, lakini hakufanya makubwa kama mwanzo, alipachika bao dakika ya 72 kwa mkwaju wa penalti.

Lilikuwa ni bao la kusawazisha kwani Namungo ilipata bao la kwanza ambalo nalo lilifungwa kwa mkwaju wa penalti na beki wa kulia wa zamani wa Yanga, Djuma Shaaban, ambaye msimu huu amesajiliwa na timu hiyo ambayo ilikuwa inacheza nyumbani, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Raia huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambaye amesajiliwa msimu huu na Tabora United akitokea Al Murooj ya Libya, hakucheza katika mechi ya kwanza ambayo timu hiyo ilicheza dhidi ya Simba, Agosti 18, mwaka huu, kutokana na kutokuwa na vibali.

Straika huyo alifunga mabao 17 msimu wa Ligi Kuu 2018/19, akishika nafasi ya tatu kwenye ufungaji bora chini ya Salum Aiyee wa Mwadui aliyemaliza na mabao 18, mshindi wa kiatu cha dhahabu msimu huo akiwa na Meddie Kagere wa Simba aliyetupia mabao 23.

Katika mechi hiyo ambayo Tabora United ilitoka na ushindi wa mabao 2-1 ikiwa ugenini, baada ya kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba, bao la ushindi liliwekwa wavuni na Salim Chuku dakika za majeruhi.

Baada ya kuanza mechi ya kwanza kwa kipigo, ikiwa nyumbani, Kocha Mkuu wa Namungo, Mwinyi Zahera, alisema Tabora United walikuwa na bahati tu na wala hawakuwafunga kwa kuwazidi mbinu au ufundi.

„Siwalaumu wachezaji wangu katika mchezo huu, walicheza vizuri, walijitolea, ni makosa machache ambayo tumefanya ndiyo wenzetu waliyatumia, sisi tumepata nafasi nyingi sana kuliko wao, lakini hatukuzitumia vizuri, nadhani Tabora United walikuwa na bahati tu," alisema kocha huyo Mkongomani.

Kocha Mkuu wa Tabora United, Mkenya, Francis Kimanzi, alisema mchezo dhidi ya Simba ulimpa somo kubwa, ndiyo maana ameshinda katika mechi hiyo.

„Ulikuwa mchezo mgumu, Namungo ni wazuri, wana utimamu mzuri wa mwili, na wachezaji wana maumbile makubwa makubwa kuliko wangu, ila tulitoka kucheza mechi ngumu dhidi ya Simba na ule mchezo ulitusaidia sana," alisema.



Sven-Goran Eriksson

### Fadlu akoshwa na Mukwala, Mashaka

INATOKA UK. 24

timu nzuri nimeshawahi kuiona, tena ikiwa nyumbani inakuwa na mashabiki wengi uwanjani, msimu uliopita ilifika mbali kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, lakini hata hivyo Simba ni timu kubwa si Tanzania tu bali Afrika nzima, na sisi kwenye mchezo wa marudiano tutakuwa na mashabiki wengi nadhani zaidi yao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, tutafanya vizuri," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Wakati huo huo, straika wa Simba, Valentino Mashaka, anaongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa na mabao mawili mpaka sasa, huku kiungo mshambuliaji wake, Jean Charles Ahoua naye akiongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao, akiwa na ‚asisti' tatu mpaka sasa ambapo ligi imeingia raundi ya pili, akifuatiwa na Mohamed Hussein ‚Tshabalala' ambaye ana ‚asisti' mbili.

# Mauti ilivyomkuta Kocha Goran Eriksson

**Sunne, Sweden**

KOCHA wa kwanza ambaye si Muingereza kuinoa England, Msweden Sven-Goran Eriksson, ameiaga dunia jana asubuhi wakati akipigania uhai wake dhidi ya ugonjwa wa saratani.

Eriksson ambaye aliwaongoza ‚Simba Watatu' hao (Three Lions) hadi robo fainali katika michuano mitatu mikuu katika kipindi chake cha miaka mitano kama kocha kati ya 2001 na 2006, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 76.

Januari mwaka huu alisema alikuwa na mwaka „bora zaidi" wa kuishi baada ya kugundulika kuwa na saratani.

Watoto wake, Lina na Johan, jana Jumatatu walisema: "Baba yetu Sven-Goran Eriksson alilala kwa amani nyumbani kwake Bjorkefors nje ya Sunne asubuhi ya leo (jana). Kwa muda mrefu amepigana kwa ujasiri na ugonjwa wake, lakini sasa umefikia mwisho.

"Baba alitueleza mwanzoni mwa mwaka huu, kuhusu ugonjwa wake mbaya na akapokea majibu ya kushangaza kutoka kwa marafiki na mashabiki wa soka kote Ulaya.

"Alialikwa na timu kadhaa za kandanda nchini Uingereza, Italia, Ureno na Sweden. Walishiriki mapenzi yao kwa mpira wa miguu na kwa baba.

„Ilikuwa jambo lisiloweza kusahaulika kwake na kwetu. Alionesha shukrani na furaha yake na kusema kwamba maneno kama hayo mazuri hutamkwa tu wakati mtu amekufa.

"Tunatumai kuwa utamkumbuka Svennis kama mtu mzuri na ambaye alikuwa hadharani na nyumbani pamoja nasi kila wakati."

Kocha huyo raia wa Sweden, enzi za uhai wake alizinoa klabu 12, ikiwamo Manchester City, Leicester, Roma na Lazio, huku akishinda mataji 18. Eriksson pia aliwahi kuinoa Mexico, Ivory Coast na Ufilipino.

Baada ya kustaafu kama mchezaji akiwa na umri wa miaka 27, Eriksson alianza kazi yake ya ukocha na Degerfors mnamo 1977 kabla ya kujiunga na timu ya Gothenburg ya Sweden, ambapo alishinda ubingwa wa Sweden, Kombe la Sweden mara mbili na Kombe la Uefa 1982.

Michezo

Jumanne Agosti 27, 2024

Nipashe



**Mauti ilivyomkuta Kocha Goran Eriksson** UKURASA 23

UNALALAJE?...



Wachezaji wa Simba, wakishangilia bao la kwanza la Steven Mukwala (wa pili kulia), aliyeifungia timu hiyo kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Bara wakati wakishinda 4-0 dhidi ya Fountain Gate, kwenye mchezo uliochezwa juzi katika Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fadlu akoshwa na Mukwala, Mashaka

## ●●● Asema sasa wanakuja, atangaza kuigeukia Al Ahly Tripoli CAF, wenyewe waahidi mabao zaidi...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, akiwamwagia sifa mastraika wake, Steven Mukwala na Valentino Mashaka, kwa kusema sasa wameanza kuiva, straika huyo raia wa Uganda, amewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, kutarajia mabao mengi zaidi kutoka kwake.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate uliochezwa juzi katika Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, Mukwala alishangaa jinsi mashabiki walivyoshangilia kwa nguvu bao lake kitu ambacho amesema hajawahi kukishuhudia kabla.

Mukwala alifunga bao la pili katika mechi hiyo ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ikishinda mabao 4-0 na kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

"Nafurahi kwa kufunga bao la kwanza nikiwa na jezi hii ya Simba, ninatarajia sasa mambo mengi mazuri na mabao mengi yatakuja.

**"Kusema kweli nimejisikia furaha sana kufunga bao mbele ya umati kama ule na unashangilia kwa nguvu ni jambo ambalo sikutarajia, ni geni machoni mwangu, lakini limenipa faraja sana, inanifanya niendelee kujituma zaidi ili niwape furaha zaidi," alisema Mukwala aliyesajiliwa msimu huu akitokea, Asante Kotoko ya Ghana.**

Naye Kocha Mkuu, Fadlu alisema kitu ambacho amefurahi zaidi katika mchezo wa juzi, ni kuona mastraika wake wote wawili, Mukwala na Mashaka wamefunga.

"Kilichonifurahisha leo ni mastraika wangu wote leo kufunga, na hii hiki ndicho ninahitaji kila eneo kuwa na mashindano ya wachezaji wenyewe kwa wenyewe.

"Mchezaji anafunga, anatoka anaingia mwingine anafunga, hivyo ndivyo inavyotakiwa hata kwenye nafasi zingine," Fadlu alisema na kuongeza;

"Tuna pointi sita, mabao saba, na ,clean sheet', wakati mwingine tunahitaji zaidi, tuna matarajio makubwa, lakini kwa hili tumeridhika."

Alisema kwa sasa akili yake imegeukia kwenye michezo ya kimataifa ambapo timu yake ina mchezo wa mechi ya raundi ya kwanza dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya.

"Sasa tunageukia michuano ya kimataifa, tutapambana na Al Ahly Tripoli, ni

INAENDELEA UK. 23

# Job arejeshwa Stars, Samatta, Msuva waachwa

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Hemed Suleiman ,Morocco', amemrejesha beki wa Yanga, Dickson Job kwenye kikosi hicho, huku akimwacha nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta na mshambuliaji hatari wa kuzifumania nyavu, Simon Msuva.

Job hakuwa sehemu ya kikosi cha Stars katika mechi kadhaa zilizopita na kuzua minong'ono kwa mashabiki wa soka nchini kutokana na ubora wake alionao kwa sasa akiwa na kikosi cha Yanga, lakini jana wakati akitangaza wachezaji 23, watakaocheza mechi mbili za kusaka tiketi ya kufuzu fainali ya Mataifa ya Afrika 2025, dhidi ya Ethiopia na Guinea, alimjumuisha.

Akizungumza kwenye ofisi za Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Morocco alisema wachezaji aliowateua watakwenda kucheza michezo miwili ya kufuzu AFCON dhidi ya Timu ya Taifa ya Ethiopia, utakaochezwa nchini, Septemba 4, na dhidi ya Guinea, utakaochezwa Ivory Coast, Septemba 10, mwaka huu.

„Tunajiandaa kufuzu AFCON 2025, nimechagua kikosi cha wachezaji 23 ambacho kitacheza mchezo wa kwanza dhidi ya Ethiopia Septemba 4, Dar es Salaam na mchezo wa pili utakuwa dhidi ya Guinea, huu tutachezea nchini Ivory Coast," alisema Morocco.

Kuhusu kutomuita Samatta kwenye kikosi chake, Morocco alisema hajamjuisha kutokana na changamoto alizokuwa nazo na kudai atamuita wakati mwingine.

„Samata bado ni mchezaji wa timu ya taifa, nilizungumza naye alikuwa na changamoto zake binafsi, nitakapomhitaji atakuja," alisema Morocco.

Kwa upande wa Msuva, Morocco alisema amemwacha amalizane na timu ambayo inamhitaji kipindi hiki, na kudai akipata

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042